

**Amber** Lulu kagoma kumtaja aliyempa ujauzito

UKURASA 20



**Arteta:** Nina imani na Aubameyang

UKURASA 21

MAISHA

Februari 28, 2021 Nipashe Baba, Mama na Mwana *Jumapili*



Kweli tunawatakia mema mabinti?

Ukurasa 10



MAISHA NI NYUMBA

Mambo muhimu ya kufahamu kabla ya kuuza nyumba yako

Ukurasa 15



HARU




UKURASA 9


# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Februari 28, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0580505

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Maajabu ya panya kubaini kifua kikuu

• **Waonyesha** uwezo na ufanisi mkubwa, Mganga Mkuu wa Serikali atoa neno... *Endelea ukurasa 4*



Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, akiwa amembeba panyabuku aitwae Justine, ambaye alitumia dakika tano kubaini sampuli sita za vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu kutoka katika makohozi 60, alipotembelea mradi wa kutambua kifua kikuu kwa kutumia panya katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), mkoani Morogoro. **PICHA: YASMINE PROTUS**

## Bashiru afichua alivyopata uteuzi

UKURASA 2

## Kijana alivyopambana na mamba saa 2 ziwani

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** MWAMEJA AMVULIA KOFIA MANULA UK.23

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Kijana alivyopambana na mamba kwa saa 2 ziwani

**Na Gurian Adolf,** NKASI

MKAZI wa Kijiji cha Kabwe wilayani Nkasi mkoani Rukwa, Thomas Kasagama (23), amenusurika kifo baada ya kupambana na mamba kwa saa mbili ndani ya maji.

Tukio hilo lilitokea Februari 25 majira ya saa 11 jioni baada ya kijana huyo kufika pembeni ya Ziwa Tanganyika na kuanza kuoga bila kuchukua tahadhari dhidi ya wanyama wakali.

Akizungumza kwa tabu katika Kituo cha Afya Nkomolo mjini Namanyere anakoendelea kupata matibabu, kijana huyo alisema kuwa muda mfupi baada ya kuanza kuoga, ghafla aliibuka mamba kwenye maji na kumvamia, aliangukia ndani ya ziwa.

Alisema baada ya kugundua kilichomvamia ni mamba, aliamua kuogelea na kuelekea sehemu yenye kina kirefu cha maji, akiamkini mamba hana uwezo mkubwa wa kumdhuru mtu aliye katika kina kirefu cha maji.

Kasagama alisema kuwa alipokuwa kwenye maji ya kina kirefu, mamba huyo alimfuata na akabahatika kumkamata miguu ya mbele na kumpindua juu chini na kumshika kwa nguvu huku akipiga kelele kuomba msaada.

"Nilipiga yowe na watu walifika, lakini kwa kuwa walikuwa hawana silaha yoyote, wakashindwa kuingia ndani ya maji wakihofia maisha yao.

"Walianza kupiga kelele huenda mamba angeogopa, lakini tuliendelea kuvutana naye mpaka alipochoka ndipo akaniachia.

"Baada ya mamba huyo kuondoka, ndipo nilipata msaada wa watu waliokuwa wakipiga kelele nikiwa tayari nimejeruhiwa sana kwenye mguu na mbavu za kushoto.

"Walinipeleka hospitalini, na baadaye gari la wagonjwa lilinisafirisha mpaka makao makuu ya wilaya, ninaendelea na matibabu hapa," alisimulia.

Mganga wa zamu wa Kituo cha Afya Nkomolo, Adelina Kizila, alisema mgonjwa huyo anaendelea vizuri na kwamba afya yake imeimarika tofauti na alipofikishwa katika kituo hicho.

Diwani wa Kabwe, Asante Lubisha, alisema kuwa baada ya kupata taarifa hizo, aliwasiliana na Idara ya Afya wilayani kuhakikisha gari la kubebea wagonjwa linapatikana na kufika kwa wakati ili kuokoa maisha ya kijana huyo.

Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, akizungumzia tukio hilo, aliwaonya wakazi wa vijiji vya mwambao wa Ziwa Tanganyika kwenda kuoga ziwani kwa kuwa ni hatari kwa maisha yao.

Alisema wenye tabia ya kwenda kuoga ziwani, wanahatarisha maisha yao kwa kuwa sasa kuna ongezeko kubwa la wanyama wakali hasa mamba na viboko kwenye ziwa hilo.



Rais Dk. John Magufuli, akimwapisha Dk. Bashiru Ally Kakurwa, kuwa Balozi na Katibu Mkuu Kiongozi, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Bashiru aanika alivyopata taarifa za uteuzi wa JPM

**Na Romana Mallya**

KATIBU Mkuu Kiongozi, Balozi Bashiru Ally, amebainisha alivyopata taarifa za uteuzi wa nafasi hiyo kupitia mitandaoni ya kijamii wakati akijiandaa kufanya kazi maalum za Chama Cha Mapinduzi (CCM), alizopewa na Rais John Magufuli.

Balozi Bashiru ambaye kabla ya uteuzi huo alikuwa Katibu Makuu wa CCM, aliteuliwa juzi na Rais Magufuli kushika nafasi hiyo iliyokuwa wazi baada ya Balozi John Kijazi kufariki dunia katikati ya mwezi huu.

Akizungumza baada ya kuapishwa Ikulu Dar es Salaam jana, Balozi Bashiru alisema hawezi kuzungumza mengi kwa sababu kuu mbili, akizitaja:

"Kwanza ni mazingira ambayo nimepata uteuzi huu. Mheshimiwa Rais ulinipa kazi ambazo kwa ratiba zingechukua mpaka mwezi mzima wa tatu (Machi) na tukaagana na ilikuwa niondoke kesho (leo) au keshokutwa (Jumatatu) kwenda kufanya kazi uliyonielekeza ndani ya chama.

"Jana (juzi) jioni, nikiwa ninasoma mafaili yangu, ninapata taarifa kupitia kwenye mitandao kwamba umeniteua. Mshtuko huo hauniwezeshi kusema mengi, bado ninatafakari sana, nitafanya nini? Nitafanya vipi kukidhi matarajio yako kwa imani uliyonipa kwa mfululizo?"

Balozi Bashiri aliwaomba Watanzania wamwombee ili akidhi matarajio ya Rais katika majukumu hayo mapya.

"Ninamwomba Mungu anisaidie. Sababu ya pili ni mila, maadili, miiko ya kazi hii mpya. Upande mmoja balozi, upande mwingine Katibu Mkuu Kiongozi.

"Kwa mila, desturi, maadili na miiko ya utamaduni wa kazi hizi, siyo kazi ya maneno maneno! Ni za kusikiliza, kujifunza, kuchambua, kuamua na kutenda," alisema.

Balozi Bashiru, mhadhiri wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alimwahidi Rais Magufuli kuwa hatamwangusha, akimwomba Mungu amsaidie.

Aliwaomba viongozi wakuu wa mihimili ya serikali wawe walimu wake na kuahidi kuwa mwepesi wa kujifunza.

"Nilikuwa nikifuatilia maelekezo yako ili tuweze kuyasimamia ndani ya chama kupitia serikali. Yale niliyokuwa nikisimamia na kupeleka kwa Waziri Mkuu, ndiyo hayo nimekabidhiwa leo (jana).

"Kati ya mambo (Rais) uliyosema Dar es Salaam, la kwanza ni umuhimu wa mawasiliano ndani ya serikali na mawasiliano kati ya serikali na umma.

"Tutalisimamia ili kuhakikisha serikali inafanya kazi kama timu moja kupitia utumishi wa umma, lakini pia idara, taasisi, wizara na mamlaka mbalimbali serikalini zinatoa taarifa kwa wakati na kwa usahihi kwa wananchi, ili wananchi wajue serikali yao inafanya nini," aliahidi.

Balozi Bashiru pia alisema Rais Magufuli tangu ameingia madarakani amekuwa akisisitiza umuhimu wa uzalendo, uadilifu na utumishi kwa wananchi hasa katika kutatua kero zao.

"Ninakuahidi nitalisimia hili kwa sababu umelisimamia kwa nguvu zote. La mwisho ni umuhimu wa kusimamia haki na umesisitiza wajibu wa kila mmoja wetu.

"Umezungumzia kodi au tozo mbalimbali, kuhakikisha utaratibu wa kisheria na misingi ya haki inazingatiwa na kusimamia uwajibikaji ili nchi ipige hatua ya kutosha, nitalisimamia.

"Mungu amemchukua Balozi Kijazi lakini ametuachia hazina kubwa. Alikuwa mchapakazi na mpole, siwezi kusema nitakuwa kama Balozi Kijazi, lakini ninamwomba Mungu anibariki niendeleze yale aliyokuwa anafanya katika uongozi wake," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Spika Job Ndugai, Naibu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema chombo hicho kitampa ushirikiano Balozi Bashiru.

"Nikuombe ule ushirikiano ambao tulikuwa tunauzungumza aliokuwa nao mtangulizi wako, tunautarajia kutoka kwako kwa maana ya kuwa kiungo kati ya serikali na Bunge.

"Tunafahamu mambo mengi kabla ya kuletwa bungeni, yanapita mikononi mwako, tunaamini ushirikiano utaendelea kuwapo," alisema.

Alisema Bunge litaendelea kutoa ushirikiano ambao umekuwapo na kwamba Rais amekuwa akiwaheshimu na wataendeleza ushirikiano huo.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahimu Juma, alisema amemfahamu Balozi Bashiru kwa muda mrefu kwa sababu siku zote amekuwa mwanafunzi wa Hayati Mwalimu Julius Nyerere, Ali Hassan Mwinyi (Rais awamu ya pili), Benjamin Mkapa (Rais awamu wa tatu), Jakaya Kikwete (Rais wa awamu ya nne) na Rais Magufuli.

"Mahakama tunategemea watumishi wa umma, soko letu kubwa la watumishi wa umma linatoka serikali kuu, tumekuwa tukifanya kazi kwa ukaribu sana na serikali kuu, laini ya mawasiliano yetu kati ya mahakama na serikali kuu tutaendelea kuiboresha," alisema.

Katika hatua nyingine, jana Rais Magufuli alishiriki mkutano wa 21 wa kawaida wa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ulioongozwa na Rais wa Rwanda, Paul Kagame, ambaye ni Mwenyekiti wa jumuiya hiyo.

HABARI KITAIFA

# Tanzania yajipanga kuuza umeme nje

**Na Joseph Mwendapole,** MOROGORO

SERIKALI imetangazaa kuwa bei ya umeme itashuka na itakuwa na akiba ya kuziuzia nishati hiyo nchi jirani baada ya kukamilika kwa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere Juni mwakani.

Hayo yalibainishwa jana mkoani Morogoro na Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, alipofungua mkutano wa siku mbili wa wahariri na waandishi wandamizi. Mkutano huo wa siku mbili umeandaliwa na Shirika la Umeme (TANESCO) kwa ajili ya kutembelea bwawa hilo litakalokuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 2,150.

Waziri Kalemani alisema bei ya umeme itashuka kwa sababu uzalishaji wa nishati hiyo kwa njia ya maji ni rahisi kulinganisha na uzalishaji kwa njia zingine kama mafuta.

Alitoa mfano uzalishaji wa uniti moja ya umeme kwa njia ya maji ni Sh. 30 hivyo kuna neema ya gharama ndogo ya umeme kwa Watanzania mara tu mradi huo utakapokamilika.

Alisema mpaka kufikia mwaka 2023, Tanzania kupitia vyanzo vyake mbalimbali vya kuzalisha umeme, itakuwa na uwezo wa kuzalisha megawati 4,881 wakati mahitaji hayatazidi megawati 2,700 kwa wakati huo.

Alisema nchi itakuwa na akiba ya megawati 2,100 ambazo zinaweza kuuzwa kwa nchi jirani zenye uhaba wa nishati hiyo.

Waziri Kalemani alipongeza uamuzi wa Rais John Magufuli kujenga bwawa hilo ambalo litaihakikishia nchi kuwa na umeme wa kutosha na wa uhakika, hivyo kuwavutia wawekezaji wengi kuwekeza nchini.

Alisema ujenzi wa bwawa hilo haujasababisha na wala hautasababisha uharibifu wowote wa mazingira kwa kuwa sehemu iliyotumika ni ndogo kulinganisha na ukubwa wa eneo la Selous.

"Badala yake uzalishaji wa umeme kwenye bwawa hili utapunguza uharibifu wa mazingira kwa sababu ukataji miti kwa ajili ya mkaa utapungua sana, hivyo tunapaswa kujivunia ujenzi wa mradi huu," alisema.

Alisema imekuwa kawaida kuona maelfu ya magunia ya mkaa yakiingia mkoani Dar es Salaam kutokana na ukataji wa miti, jambo ambalo litapungua iwapo kutakuwa na umeme mwingi wa kutosha.

"Ukipiga hesabu ya magunia ya mkaa yanayotumika kwa mwaka mmoja tu, utaona namna gani mazingira yetu yanavyoharibiwa sasa, ukipiga kwa miaka 10 athari zake ni mbaya sana.

"Ndiyo maana Watanzania tuna kila sababu ya kumpongeza Rais Magufuli kwa ujasiri wake wa kuhakikisha mradi huu unatekelezwa kwa sababu faida zake ni nyingi sana kwa uchumi wetu," alisema.



Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (kushoto) na Mkuu wa Jeshi la kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Chales Mbuge, wakisaini mkataba wa makubaliano wa kukuza sekta ya Kilimo, jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Serikali yalegeza masharti ya mikopo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ametangaza kulegeza kanuni za mikopo itokanayo na asilimia 10 ya mapato ya halmashauri nchini.

Katika kanuni hizo, kwa sasa kikundi cha vijana na wanawake chenye watu watano kitapata mkopo tofauti na masharti ya awali walilazimika kuwa 10 huku kwa watu wenye ulemavu, hata mtu mmoja atakopeshwa mkopo bila kuwapo kwenye kikundi.

Jafo aliyasema hayo jana jijini hapa alipofungua mkutano wa siku tatu wa mwaka wa Chama cha Wataalamu wa Maendeleo ya Jamii. Alisema hatua hiyo imetokana na kupokea maombi mengi na malalamiko dhidi ya kanuni inayotaka kikundi lazima kuwa na watu kuanzia 10.

"Katika maeneo mengi, ni vigumu sana kuwapata watu wanaokubaliana kuwa pamoja hadi kufikia 10 na hasa kwa watu wenye walemavu, imekuwa ngumu kuwapata 10 wenye ulemavu wa aina moja. Sasa hata mtu mmoja mwenye ulemavu anaweza kukopa," alisema. Alisema kuanzia sasa maofisa maendeleo ya jamii watapata nakala za kanuni mpya zitakazokwenda kuwaongoza katika kutekeleza majukumu yao katika maeneo yao ya kazi.

Jafo alisema wamefanya marekebisho kuhakikisha urejeshwaji wa mikopo hiyo unaimarika na sasa watatenga fedha kwa ajili ya ufuatiliaji wa mikopo. Alisema halmashauri zimetengwa katika makundi ambapo halmashauri zenye mapato yasiyozidi Sh. bilioni moja, lazima zitenge kila mwezi kiasi cha Sh. 500,000 hadi Sh. milioni moja.

"Wakati katika halmashauri zenye mapato kuanzia Sh. bilioni moja hadi mbili, wao watatenga kiasi cha Sh. milioni moja hadi Sh. milioni 1.5.

Kwa halmashauri zinazokusanya kuanzia Sh. bilioni tano na kuendelea, lazima watenge kiasi cha Sh. milioni tano kila mwezi kwa ajili ya kuwawezesha maofisa maendeleo ya jamii kuvifuatilia hivyo vikundi.

"Ninasisitiza fedha hizi ni kwa ajili ya marejesho ya mikopo na siyo fedha zilizotengwa. Kwa hiyo kama hufuatilii vikundi hivyo au hakuna marejesho ya vikundi, fedha hizi zisitengwe, tunafanya hivi ili ufuatiliaji uimarishwe," alisema.

Waziri huyo alibainisha kuwa kwa miezi sita ya mwaka wa fedha 2020/21, tayari serikali imetumia Sh. bilioni 24 na kwa kipindi cha miaka mitano, serikali imetumia Sh. bilioni 143 kutoa kwa vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu nchini. Aliwashukuru wataalamu wa maendeleo ya jamii kwa kazi kubwa wanayoendelea kufanya nchini na kubainisha kuwa kwa sasa kitengo hicho kinazidi kuimarika tofauti na awali.

Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Idara kuu ya Maendeleo ya Jamii, Patrick Golwike, alisema wataalamu hao wamekutana kwa siku tatu kwa lengo la kujadili namna ya kuboresha taalamu hiyo katika maeneo yao ya kazi.

Alisema kwa sasa wameboresha mkutano huo kwa kuwa awali walikuwa wakihudhuria wakuu wa idara pekee na sasa wanashirikisha wataalamu wote hadi ngazi za chini ili kuboresha taaluma. Katika mkutano huo, wamechagua viongozi wapya watakaoongoza wataalamu wa chama kwa kipindi kingine, nafasi ya mwenyekiti akishinda Angela Mvaa, Makamu Mwenyekiti Dk. Regina Malima na Katibu Mkuu Daniel Wambura.

## Neema yatua wajasiriamali wa Ruangwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amekabidhi vifaa mbalimbali vyenye thamani ya Sh. milioni 357 kwa vikundi vitano vya wajasiriamali vilivyotolewa kupitia mkopo na Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa ikiwa ni asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri.

Vilevile, Majaliwa amepokea msaada wa madawati 100 yenye thamani ya Sh. milioni 10 kutoka kampuni ya vinywaji baridi ya Coca-Cola Kwanza ikiwa ni kuunga mkono jitihada za serikali katika kuboresha Sekta ya Elimu nchini.

Waziri Mkuu alikabidhi vifaa hivyo jana kwenye viwanja vya Shule ya Msingi Likangara wilayani Ruangwa na kuwataka wanufaika wa mikopo hiyo wakaitumie kama ilivyokusudiwa na wahakikishe wanarejesha kwa wakati.

Alitumia fursa hiyo kuipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa kwa kuamua kutoa mikopo ya vifaa mbalimbali kwa wajasiriamali na akaitaka ihakikishe inawasimamia vizuri wanufaika hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Frank Chonya, alisema halmashauri yao imeendelea kutenga na kutoa mikopo kwa vikundi vya ujasiriamali vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 ya makusanyo ya mapato ya ndani.

Alibainisha kuwa mwaka 2020/21, halmashauri imetoa mikopo mikubwa yenye thamani ya Sh. milioni 357 ambazo wanavikundi wamenunua vifaa kwa ajili ya shughuli zao na wengine wameanzisha biashara ndogo.

Alisema halmashauri ilifanya utafiti na kuunda vikundi vitano vya kimkakati ambavyo vimepewa mikopo yenye thamani ya Sh. milioni 319.91," alisema.

Baada ya kupokea vifaa hivyo, wanufaika hao waliishukuru serikali kupitia Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo kwa kuamua kuwakopesha vifaa kwa kuwa vitaboresha shughuli zao za ujasiriamali huku wakiahidi kurejesha fedha hizo kwa wakati ili wananchi wengine wanufaike.

Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma wa Coca-Cola Kwanza, Salum Nassor, alisema kampuni yao imekabidhi madawati 100 yenye thamani ya Sh. milioni 10.

Nassor alisema wametoa msaada huo ili kuunga mkono juhudi za serikali katika kuboresha elimu nchini.

# Maajabu ya panya katika kugundua TB

**Na Yasmine Protace,**
MOROGORO

KIFUA kikuu (TB) kimekuwa moja ya magonjwa tishio duniani kutokana na mamilioni ya watu kukumbwa na maradhi hayo na wengine kupoteza maisha.

Takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinaonyesha kuwa mwaka jana, watu waliokuwa wanaogua kifua kikuu wanakadiriwa kuwa milioni 10 wakiwamo wanaume milioni 5.6, wanawake milioni 3.2 na watoto milioni 1.2. idadi hiyo ni ongezeko kwa asilimia 10 kulinganisha na mwaka 2018.

Kwa upande wa vifo, takwimu za WHO zinaonyesha kwamba kwa mwaja jana, watu waliopoteza maisha kutokana na TB ni milioni 1.4 wakiwamo 208,000 waliokuwa na maradhi ya Ukimwi.

Nchini Tanzania, kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu na Ukoma (NTLP), ugonjwa huo ni namba tatu katika kugharimu maisha ya watu baada ya malaria na Ukimwi.

Hata hivyo, kumekuwa na matokeo chanya katika kuudhibiti kutokana na kupungua kwa wagonjwa kila mwaka. Mwaka 2018 wagonjwa walipungua kutoka 306 kati ya watu 100,000 hadi 253 kwa 100,000. Vifo pia vimepungua kutoka 58 hadi 40 kwa idadi hiyo hiyo ya watu.

Matokeo hayo yanaonyesha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika malengo yake ya kupambana na tatizo hilo ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Millenia (SDG) ya Umoja wa Mataifa (UN). Kupitia malengo hayo, UN inaazimia kuwa ifikapo mwaka 2030 ugonjwa huo uwe umetokomezwa.

Katika kufanikisha azma hiyo, kumekuwa na mikakati na mbinu mbalimbali ikiwamo watu kuwahi kupima na wanapobainika kuwa na vimelea au maambukizi, waanze tiba mapema kwa kuwa ni ugonjwa unaotibika na pia kuzuilika.



Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Majibu (wa pili kulia), akimsikiliza Mkuu wa Mradi wa Kutambua Kifua Kikuu kwa Kutumia Panya, Dk. Georgies Mgode (kulia), wakati alipotembelea mradi huo, katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), mkoani Morogoro. **PICHA: YASMINE PROTUS**

**TEKNOLOJIA YA PANGA**

Tanzania, kama zilivyo nchi zingine, imekuwa na mbinu mbalimbali na miaka ya karibuni, iliazisha teknolojia ya kutumia panya buku katika kubaini TB ambayo imeonyesha maajabu na ufanisi mkubwa.

Wanyama hao wanatumika kubaini sampuli za wagonjwa wenye dalili za ugonjwa huo ili kuongeza uwezo wa kutambua vimelea hasa pale njia zingine zinapokuwa zimeshindwa.

Hayo yalibainika jana wakati wa ziara ya Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, alipotembelea kitengo cha APOPO katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) mjini hapa.

"Napongeza mapinduzi kutoka kwa wanasayansi wazalendo ya kuwawezesha panya buku wa SUA kunusa na kubaini vimelea vya kifua kikuu katika sampuli za makohozi yanayoletwa hapa kwa ajili ya vipimo vya kifua kikuu. Kufikia mwaka huu, huduma hii itazifikia zaidi ya hospitali 100 nchini," alisema.

Prof. Makubi pia aliwapongeza watafiti wa SUA kwa hatua ambayo wamefikia katika baada ya kukitembelea na kuona wamekuwa wakifanya ugunduzi wa vimelea vya kifua kikuu kwa kutumia panya hao.

Aliongeza kuwa wamewafundisha na kusambaza hiyo teknolojia katika nchi mbalimbali kama vile Msumbiji na Ethiopia ambako wanapima TB na kwenye nchi za Cambodia na Angola ambako wanafanyakazi ya kutambua mabomu ya ardhi.

Prof. Makubi alisema panya hao wana uwezo mkubwa wa kugundua vimelea vya TB hata kwa mtu ambaye alifanya vipimo hospitalini kama vile vya hadubuni (microscope) na mashine za kupima vinasaba mfano 'GeneXpert' na vipimo vingine na vikatoa majibu kuwa hana TB.

"Lakini panya hawa wana uwezo wa kubaini vimelea ambavyo mashine za hospitalini zinaweza zisibaini. Hii inaonyesha utumiaji wa panya hawa unaweza kusaidia kuongeza ugunduzi wa wagonjwa wengi zaidi. Panya mmoja ana uwezo wa kugundua kama sampuli ina vimelea vya kifua kikuu kwa muda wa sekunde moja, hivyo hupima sampuli za makohozi 100 kwa dakika 20.

Teknolojia hii inaweza kutumika hata kwenye upimaji wa sampuli nyingi kutoka kwenye kundi kubwa la watu kwa muda mfupi," alisema.

Prof. Makubi alishuhudia panya ajulikanae kwa jina la Justine, akipima sampuli 60 za makohozi ndani ya dakika tano na kugundua sampuli sita zenye vimelea vya kifua kikuu.

Mpaka sasa huduma hiyo inatolewa katika hospitali 74 na kubaini wagonjwa 14,680 ambao hawakugundulika kwa njia za kawaida na kusaidia wagonjwa 8,119 kuanza matibabu.

Hatua hiyo imezuia maambukizi ya kifua kikuu kwa wananchi 81,190 hadi 121,785 ambao wangeambukizwa kutokana na mgonjwa mmoja ambaye hajatibiwa anaweza kuambukiza ugonjwa huo kwa watu wa karibu naye 10 hadi 15 kwa mwaka.

"Hatua hii inanipa faraja sana nikiwa kiongozi wa sekta ya afya kwa sababu lengo la sekta hii ni kulinda afya za watu wake. Tunapopata kipimo kama hiki kinasaidia wananchi wengi kujua afya zao na matokeo yake tutaokoa wananchi wengi kwa kupata tiba na kufanya maisha yao kuwa marefu zaidi. Lakini pia tunapunguza uwezekano wa kusambaza ugonjwa huo kwa watu wengine," alisema Prof. Makubi.

Pia Mganga Mkuu aliahidi kulifanyia kazi ombi la Mkuu wa Mradi wa Kutambua Kifua Kikuu Kupitia Panya Buku, Dk. Georgies Mgode, la kuitambua teknolojia hiyo ya panya buku katika mwongozo wa kutibu kifua kikuu nchini.

Prof. Makubi aliielekeza SUA kuendelea kushirikiana na wizara na Taasisi ya Utafiti wa magonjwa ya binadamu katika kuboresha huduma za afya katika maeneo ya kubaini magonjwa, kuanza kutengeneza chanjo, kuimarisha tiba asili, kupanua utafiti za magonjwa, kutoa mchango katika kuboresha lishe za wananchi na kushirikisha sekta mbalimbali katika kuboresha huduma za afya.

Kwa upande wake. Dk. Mgode alisema kuanzia mwaka 2007 hadi Desemba, mwaka jana, mradi huo umeshapokea na kupima sampuli za makohozi 559,428 kutoka kwa wahisiwa wa kifua kikuu huku wakiongeza utambuzi wa wagonjwa kwa asilimia 40 katika maeneo ya mradi.

Alisema hiyo ikisambaa maeneo mengi nchini, Tanzania inaweza kuondokana na janga la ugonjwa huo kwa kuwa tayari Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma, unatambulika duniani kuwa mfano katika mapambano dhidi ya kifua kikuu.

Naye Makamu Mkuu wa SUA, Prof. Raphael Chibunda, alimshukuru Mganga Mkuu wa Serikali kwa kuonyesha nia ya wizara pamoja na SUA kushirikiana kuzalisha wataalamu na kufanya utafiti mbalimbali ambao utasaidia sekta ya afya.

Prof. Chibunda aliahidi kuwa SUA itaendelea kutoa mchango wake katika utafiti mbalimbali wa kuboresha huduma za afya nchini.

## HABARI KITAIFA

# Ajali ilivyokatisha maisha ya maofisa RUWASA, mwanafunzi

**Na Ndalike Sonda,** SIMIYU

WATU wanne wamepoteza maisha kutokana na ajali iliyohusisha magari mawili kugongana uso kwa uso katika Kijiji cha Dutwa wilayani Bariadi mkoani Simiyu jana.

Akithibitisha kutokea kwa ajali hiyo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Richard Abwao, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 11:30 jioni baada ya gari namba T.851 DKF Toyota Mark X lililokuwa likitokea Bariadi, kugongana na basi lenye namba za usajili T. 350 DUH aina ya Tata, mali ya kampuni ya Ngalabushi lililokuwa linatoka Lamadi kwenda Bariadi.

Kamanda Abwao aliwataja waliofariki dunia kuwa ni Castory Mambileo (35), Ofisa Ugavi wa RUWASA Mkoa wa Simiyu, Penina Naveta (38), Ofisa Utumishi wa RUWASA Mkoa wa Simiyu, Raphael Kichele (30) ambaye ni mfanyabiashara, na Ntobi Mapalala (7) mwanafunzi na mkazi wa Dutwa.

Alisema katika ajali hiyo, gari aina ya Toyota Mark X lilimgonga mtembea kwa miguu Ntobi Mapalala na kisha kugongana na basi hilo la Ngalabushi.

Baadhi ya mashuhuda wa ajali hiyo, walidai chanzo chake ni mwendokasi wa gari dogo bila kuchukua tahadhari.

Hata hivyo, Kamanda Abwao alisema chanzo cha ajali hiyo bado kinachunguzwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Simiyu.

Alitoa wito kwa watumiaji wa barabara kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepukana na matukio ya ajali.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Brigedia Jenerali, John Mbungo (kulia), akimkabidhi Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mhandisi Isaack Chanji, vifaa vya umeme vikiwamo transfoma 30 na taa 20,000 ambavyo vilikabidhiwa kwa taasisi hiyo kutoka kwa makandarasi, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa shirika hilo, Dk. Alexander Kyaruzi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# TAKUKURU yarejesha vifaa vya mamilioni TANESCO

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imelikabidhi Shirika la Umeme (TANESCO) transfoma 30 na taa 20,000, vyote vikiwa na thamani ya Sh. milioni 420, vilivyokuwa vinashikiliwa na makandarasi wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) tangu mwaka 2017.

Vifaa hivyo vilishikiliwa na makandarasi hao akiwamo M/S JV STATES GRID ELECTRICAL & TECHNICAL WORKS LTD aliyetekeleza mradi wa REA uliokamilika mwaka 2017 mkoani Kigoma.

Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Brigedia Jenerali John Mbung'o, akikabidhi vifaa hivyo Dar es Salaam jana kwa Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Isaack Chanji, alisema vifaa hivyo vilipotea kwa mbinu mbalimbali zilizofanywa na baadhi ya makandarasi waliotekeleza awamu ya pili ya mradi huo.

Alisema mbali na kurejeshwa kwa vifaa hivyo, kesi tano zimefunguliwa mahakamani kwa madai ya kusababisha hasara kwa shirika zaidi ya Sh. bilioni 2.7.

"Nimnukuu Rais John Magufuli na kauli aliyotoa Julai 22 mwaka jana akizindua majengo ya TAKUKURU Chamwino alisema "rushwa ni mbaya mno. Unakuta mwanamama analia amedhulumiwa, labda hajapata urithi wake na unakuta chombo cha TAKUKURU kipo pale wilayani."

Kiongozi huyo wa TAKUKURU alisema kutokana na maagizo hayo ya Rais, taasisi hiyo kwa mamlaka iliyopewa na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007, imeendelea kujikita katika operesheni maalum nchini kurejesha fedha na mali za wananchi wanyonge ambazo zilikuwa zimedhulumiwa.

Alisema kuwa akiwa mkoani Iringa mwaka jana, alikabidhi TANESCO vifaa ghafi vya umeme vyenye thamani ya Sh. bilioni 1.2 na aliwataja makandarasi waliotekeleza mradi huo na wanadaiwa vifaa kuvirejesha mara moja.

"Niliagiza kwamba makandarasi wanaodaiwa, wawe wamefanya marejesho ya vifaa ghafi hivyo vya umeme ndani ya siku 14.

"Wadaiwa hawa ni ambao tangu mwaka 2017 walitakiwa wawe wamewasilisha TANESCO vifaa ghafi vya umeme vilivyobaki baada ya mikataba yao kukamilika, lakini hawakufanya hivyo," alifafanua.

Alisema kuwa baada ya agizo hilo, baadhi walifika TAKUKURU kuhakiki aina na idadi ya vifaa vya umeme wanavyotakiwa kuvirejesha.

"Wakandarasi waliofika ni DERM ELECTRICS (T) LTD, M/S JV STATES GRID ELECTRICAL & TECHNICAL WORKS LTD, NAKUROI INVESTMENTS pamoja na URBAN & RURAL ENGINEERING SERVICES LIMITED," alisema.

Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa TANESCO, Chanji, aliishukuru TAKUKURU kwa kukabidhi vifaa hivyo na kusisitiza kuwa vitaongeza ufanisi wa kazi.

# Waziri aagiza matukio ya moto shuleni yadhibitiwe

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amelitaka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kushirikiana na Chama cha Skauti Tanzania kukomesha majanga ya moto kwenye shule za msingi na sekondari.

Jafo alitoa agizo hilo juzi alipozindua kampeni ya pamoja kati ya taasisi hizo inayolenga kukabiliana na majanga ya moto.

Alibainisha kuwa moja ya sababu zinazochangia kutokea kwa majanga ya moto ni baadhi ya wanafunzi kutokuwa na uelewa wa kujiepusha na majanga hayo.

"Katika siku za hivi karibuni, tumeshuhudia baadhi ya shule zikiungua kwa moto na nyingine kuteketea kabisa. Tunapaswa kuwa na elimu hii kwenye shule ili kudhibiti majanga haya," aliagiza.

Alisema kwa sasa serikali inajenga na kuimarisha miundombinu ya shule nchi nzima, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule mpya 1,000, akisisitiza kuwa kukamilika kwake lazima kuendane na elimu ya majanga mbalimbali yakiwamo ya moto.

Kuhusu makubaliano baina ya jeshi hilo na Skauti Tanzania, Waziri Jafo alisema Chama cha Skauti Tanzania kimekuwa na jukumu kubwa la kujenga uzalendo miongoni mwa vijana wawapo shuleni huku akiwataka maofisa elimu wa mikoa na halmashauri kuendelea kutoa ushirikiano kwa chama hicho, ili uzalendo uliojengeka miongoni mwao, uzidi kuimarika.

Awali, akitoa salamu za jeshi hilo, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto, John Masunga, alisema jeshi limeanzisha kikosi kazi kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Ofisi ya Rais -TAMISEMI, shabaha ikiwa ni kuhakikisha elimu ya kukabiliana na majanga ya moto inawafikia wanafunzi na kuongeza uelewa wa pamoja juu ya athari za moto miongoni mwao.

Kamishna Mkuu wa Skauti nchini, Mwantumu Mahiza, alisema chama hicho kimekuwa kikitekeleza wajibu wake kwa mujibu wa viapo vyao na kinatambua serikali inatumia fedha nyingi kwenye uwekezaji wa miundombinu ya shule, hivyo kina wajibu wa kuilinda.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Viongozi wazinduke, wafuatilie malipo ya wastaafu kwa wakati

**WIKI** hii, Rais John Magufuli alikuwa na ziara katika mkoa wa Dar es Salaam ambapo pamoja na mambo mengine, alizindua daraja la juu la Ubungo lililopewa jina la John Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi na stendi ya mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani iliyoko Mbezi Luis, iliyopewa jina la Magufuli.

Rais alihitimisha ziara hiyo ya siku tatu juzi kwa kufungua majengo ya Chuo cha Taaluma cha Polisi na kuweka jiwe la msingi kwenye kiwanda cha ushonaji wa sare za pilisi, Kurasini.

Mara baada ya kuhitimisha uwekaji jiwe la msingi, Rais, kama ilivyo ada, alihutubia Watanzania kupitia vyombo vya habari na kuwataka mawaziri kusimamia na kufuatilia suala la mafao ya wastaafu. Alizungumza jambo hilo baada ya Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Sirro, kubainisha kuwapo maofisa wa polisi wastaafu ambao hawajapewa mafao yao kwa muda mrefu.

Kutokana na taarifa hiyo, Rais alieleza kushangazwa na viongozi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, akiwamo Waziri George Simbachawene, kutokufuatilia suala hilo na kuwaacha wastaafu wakitaabika wakati haki zao zimekaliwa.

Bila kuuma maneno, Rais aliwaambia kuwa inashangaza kuona mtumishi amefanya kazi yake nzuri kwa miaka yake na bila tatizo lolote lakini badala ya kuliopwa mafao yake anasumbuka kuyafuatilia kwa muda mrefu bila mafanikio yoyote. Pia aliwahoji Waziri na naibu wake, katibu mkuu na naibu wake wanakaa ofisini bila kufuatilia matatizo ya wafanyakazi walio katika taasisi za wizara wakiwamo wastaafu ambao badala ya kufurahia matunda ya utumishi wao, wanajuta na kutaabika.

Licha ya kuwashangaa viongozi hao, Rais aliwapa mbinu kuwa ili kufanikisha jambo hilo, wanapaswa kwenda wenyewe Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) kufuatilia fedha za wastaafu hao. Alibainisha kwamba hata yeye alipokuwa waziri, alipoona jambo linakwama, alikwenda mwenyewe Hazina na kufuatilia hadi fedha zinapatikana.


Kwa kuweka hadharani suala la wastaafu, Rais magufuli amewafumbua macho Watanzania ambao baadhi yao, wakiwamo wastaafu, wamekuwa wakiitupia lawama serikali kuwa chanzo cha kutopata mafao yao, huku baadhi wakidai fedha zimekwenda kwenye ujenzi wa miradi inayotekelezwa na serikali. Rais amebainisha kuwa wanaokwamisha mafao ya wastaafu ni waajiri kwa kushindwa kuwasilisha makato ya wafanyakazi kwa wakati pamoja na kupeleka taarifa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii na Hazina. Matokeo yake ni watumishi kupata taabu baada ya kustaafu.

Tumeshuhudia wastaafu wengi kuishi maisha ya shida baada ya kustaafu huku wengine wakikumbwa na maradhi kama vile msongo wa mawazo, kiharusi na shinikizo la damu na hata baadhi kupoteza maisha. Pia katika baadhi ya familia kumekuwa na migogoro kutokana na ugomvi unaoibuka kwa madai kuwa wenzi wao wametumia vibaya mafao.

Ni vyema sasa viongozi wa taasisi mbalimbali wakasimamia masuala ya makato ya wafanyakazi na kuhakikisha yanafikishwa kwenye mifuko husika. Kwa maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama, pia wakuu wao wahakikishe wanaandaa mipango juu ya mafao ya askari na maofisa wao ili wastaabike baada ya kustaafu.

Hatua hiyo itaondoa dhana iliyojengeka, kutokana na ucheleweshaji wa mafao ya watumishi baada kustaafu, kuwa kustaafu ni sawa na adhabu kwa mtumishi aliyekoma ajira. Ni wakati sasa wa viongozi kubadilika na kuwajibika ili watumishi wawe na furaha baada ya kustaafu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

## Wazazi, walezi ni chachu kuinua kiwango cha elimu

**SHULE** za umma kuanzia msingi hadi na sekondari zinakabiliwa na changamoto ya uhaba wa walimu, hali inayochangia baadhi kukosa walimu na hasa wa masomo mbalimbali yakiwamo ya sayansi.

Wakati Serikali ikiendelea na mchakato wa kuajiri walimu wapya ili kumaliza au kupunguza uhaba wa walimu, baadhi ya wazazi nao wamebuni mbinu za kukabiliana na changamoto hiyo.

Baadhi ya wazazi na walezi katika maeneo mbalimbali wameamua kuchukua hatua za kukabiliana na tatizo hilo, kwa kuwalipa posho walimu wa kujitolea ili kusaidia kuinua kiwango cha elimu katika shule za sekondari.

Viwango vya malipo vinatofautiana wakiwamo ambao kila mmoja analipa Sh. 1,000 kila mwezi, wengine Sh. 900 kwa mwezi, ili kuhakikisha watoto wao wanafundishwa masomo yote wawapo shuleni.

Miongoni mwa wazazi hao ni wa Wilaya ya Musoma mkoani Mara, ambao wamejiwekea utaratibu huo, huku serikali ikiendelea na mikakati ya kuajiri walimu wa kutosha katika shule za umma.

Wakati wanachangia kiasi hicho, mbunge wao, Prof. Sospeter Muhongo, amejitolea kuipa kila shule posho ya Sh. 50, 000 kwa mwezi kwa shule za Nyanja, Kiriba, Nyakatende na Bugwema.

Juhudi za wazazi hao hazijaishia katika kulipa posho za walimu wa kujitolea tu, bali pia wanashiriki kwa hali na mali kujenga sekondari mpya zikiwamo za vijiji na kata mpya na pia vyumba vya madarasa kwa zile zenye upungufu.

Hatua hiyo inaonyesha namna ambavyo wanatambua kuwa shule hizo ni mali yao, wana wajibu wa kuzihudumia pale inapowezekana kwa ajili ya kuboresha kiwango cha elimu kwa watoto wao.

Aidha, hatua hiyo inaonyesha ni namna gani wazazi na walezi wanashirikishwa kwa kupewa taarifa sahihi na kuhamasishwa katika shughuli za maendeleo ya shule zao na hivyo kuwafanya wawe tayari kuzihudumia.

Kimsingi, shule za serikali ni za umma, na umma wenyewe ni wananchi, hivyo wakati serikali ikiendelea na mchakato wa kuajiri walimu zaidi, ni muhimu na utaratibu kama huo, ambao unachangia kuboresha elimu.

Mfano huo wa kutoa posho kwa walimu wa kujitolea ni wa kuigwa na wazazi na walezi kote nchini, kwa kuwa una mchango mkubwa kwenye maendeleo ya elimu kuliko kukaa pembeni na kudhani hawahusiki.

Ikumbukwe kuwa watoto wengi nchini, wanasoma shule za umma, ambazo zinatajwa kuwa uhaba wa walimu, hivyo ni wajibu wa umma kuzihudumia kadri inavyowezekana, ili ziwe na maendeleo mazuri.

Wazazi wanaoishi vijijini ambako shule za huko zinadaiwa kuwa na uhaba wa walimu, ni vyema wakajiongeza kama walivyofanya wenzao wa wilaya Musoma kwa kuja na mkakati wa kuwapa posho walimu wa kujitolea.

Hilo linaweza kwenda sambamba na kuchangia chakula kwa ajili ya watoto wao, na kuachana na dhana kwamba, serikali ilishazuia michango yote shuleni, hali ambayo inasababisha watoto wao washinde njaa.

Wataalam wa afya wanasema, kuwalisha chakula wanafunzi shuleni kunaongeza ulinzi wa kijamii, chakula na lishe kwa wanafunzi, kuimarisha mahudhurio shuleni na kukuza mchakato wa kujifunza.

Mkakati wa kulipa posho kwa walimu wa kujitolea, ujenzi wa shule, madarasa vikienda sambamba na kutambua umuhimu wa kutoa chakula kwa ajili ya wanafunzi shuleni, itakuwa ni hatua nzuri ya kuboresha elimu.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mwita Waitara, aliwahi kukaririwa na vyombo vya habari akisema, taifa lina uhaba wa walimu 80,000, huku 14,000 wakiwa ni wa sekondari na 66,000 wa shule za msingi.

Waitara alikuwa akijibu swali bungeni jijini Dodoma, kwamba, uhaba huo unatokana na sababu mbalimbali ikiwamo walimu hewa, uhamisho na kufariki dunia.

kwa kutambua matatizo hayo, ajira zilizofanywa baada ya serikali kujiridhisha zilikuwa ni za kuziba nafasi, na zinazofuata zitakuwa ni za kupunguza pengo la mahitaji halisi.

Wakati serikali ikiwa katika mchakato wa kuajiri walimu, wazazi na walezi hawana budi kubuni njia ya kukabili tatizo hilo kama walivyofanya wenzao wa wilaya ya Musoma ambao wanaendelea kupiga hatua kuboresha elimu.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Maalim Seif alikuwa zaidi ya chama



Nkwazi Mhango, Canada

**Ni mmoja wa wanasiasa waliotawala sana hasa kwenye siasa za upinzani na visiwani. Aligombea urais wa Zanzibar kwa miaka 25 kama tutaanzia mwaka 1992 uliporuhusiwa mfumo wa vyama vingi nchini, aligombea mwaka 1995, 2000, 2005, 2010 2015, na 2020 jumla mara sita hadi anakufa mwaka 2021.**

KWA wanaomfahamu vizuri Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, watakubaliana nami kuwa makala moja hata kitabu, havitoshi kumwelezea.

Katika safu ya leo, tutajaribu japo kumdurusu kwa ufupi ili lau kuambua somo tunalopata kutokana na kifo chake na mustakabali wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Kimsingi, Hamad, alivyokuwa akijulikana kama Maalim Seif, alijikita kwenye siasa za visiwani huku akitumia vyama vilivyoundwa Tanzania Bara.

Hakuna ubishi. Hamad alikuwa mmoja wa wanasiasa nguli nchini hasa kwenye siasa za upinzani na hata ung'ang'anizi hasa ikizingatiwa kuwa anaweza kuingia kwenye historia ya Tanzania kama mtu aliyegombea urais mara nyingi kuliko mtu yeyote tena bila kuupata.

Ni mmoja wa wanasiasa waliotawala sana hasa kwenye siasa za upinzani na visiwani. Aligombea urais wa Zanzibar kwa miaka 25 kama tutaanzia mwaka 1992 uliporuhusiwa mfumo wa vyama vingi nchini, aligombea mwaka 1995, 2000, 2005, 2010 2015, na 2020 jumla mara sita hadi anakufa mwaka 2021.

Ukimwita mwanasiasa king'ang'anizi au mwenye maslahi fulani binafsi, unaangalia hili la kugombea mara nyingi kana kwamba hakuna wengine wenye uwezo wa kufanya hivyo baada ya kutimuliwa toka Chama Cha Mapinduzi (CCM). Kutokana na hulka hii, ilifikia mahali ikawa vigumu kutofautisha kati ya Hamad na CUF kama ambavyo ilikuja kuwa kwa viongozi wengine wa upinzani ambao hufanya vigumu kuvitofautisha kati yao na vyama vyao ambavyo walivigeuza kama mashamba yao au mali binafsi.

Historia ya Hamad inaanza pale alipoteuliwa kwenye utumishi wa umma na serikali ya awamu ya kwanza Visiwani ambayo ilihitaji wataalamu baada ya kufanya mapinduzi. Maalim Seif kama alivyokuja kujulikana, alikuwa na dhamira ya kuwa Mwalimu. Hata hivyo, alibadilisha mwelekeo baada ya kuteuliwa.

Ili kufanikisha lengo lake, Hamad alianzia siasa zake ndani ya CCM kabla ya kumgeuka aliyemteua kwenye ulaji, marehemu Aboud Jumbe alipofichua mbinu yake ya kutaka serikali huru ya Zanzibar. Hata hivyo, Hamad naye aliishia kutemwa toka CCM ndipo akaanzisha chama cha Civic Union Front (CUF) pamoja na James Mapalala (marehemu) ambaye baadaye alimnyang'anya chama kabla naye kunyang'anywa na Profesa Ibrahim Lipumba hali iliyomlazimisha kukimbilia chama cha Alliance for Change and Transparency (ACT)-Wazalendo baada ya kujaribu kukirejesha chama mikononi mwake bila mafanikio.

Baada ya pigo hili, wengi walidhani ulikuwa ndio mwisho wa Hamad. Kabla ya kuwaacha hoi pale alipogombea tena kupitia chama chake kipya na kufanikiwa tena kurejea kwenye ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Visiwani, ambayo kimsingi, ilitokana na Maridhiano au Mwafaka aliouasisi Hamad mwenyewe na kufanikiwa kuwa Makamu wa Kwanza wa Rais, cheo ambacho hakikuwahi kuwapo awali.

Hapa kuna swali. Je, huu ndiyo mwisho wa nafasi hii ambayo wapo wanaoiona kama ya upendeleo kwa upinzani hasa ulioogozwa na Hamad Visiwani? Maana aliyeongoza vuguvugu ni Hamad hata bila kuwa na chama. Rejea alivyohamia ACT-Wazalendo na kuidhoofisha CUF Visiwani, Mwalimu Julius Nyerere aliwahi kusema kuwa hakuna aliye maarufu zaidi ya chama. Ni zama zile, kwani ukiangalia historia ya Hamad Visiwani, utagundua kuwa alikuwa zaidi ya chama.

Kutokana na umaarufu wake na alivyoendesha siasa zake, hakuna shaka kuwa alijitengenezea marafiki na hata maadui. Umaarufu wa Hamad ulianza kuvuka mipaka ya Zanzibar pale alipoteuliwa na Aboud Jumbe (Rais wa Awamu ya Pili Zanzibar- sasa marehemu) na kumgeuka hadi kumchomea utambi hadi akaondoka madarakani.

Baada ya hapo, Hamad aliendelea kukwea hadi kufikia kuteuliwa kuwa Waziri Kiongozi. Hata hivyo, aishiye kwa upanga atakufa kwao. Kama ilivyokuwa kwa Jumbe, Hamad alijikuta akitimliwa chamani hadi kukimbilia kwenye upinzani ambako alianzisha CUF akiwa na Mapalala kabla kumgeuka, kumwengua na kuchukua chama.

Kama ilivyokuwa kwenye kesi ya Jumbe, dhambi ile ile ilizidi kumwandama Hamad kwani naye alijikuta akienguliwa na kutupwa nje ya CUF kiasi cha kukimbilia ACT-Wazalendo ambacho chini yake kulitokea sintofahamu pale ACT-Wazalendo ilipomuunga mkono mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kwenye uchaguzi uliopita huku kikimpa mgongo mgombea wake Bernard Membe.

Unaweza kumwita Hamad mwanasiasa kigeugeu kisiasa hata kama alikuwa na msimamo kwenye mambo mengine. Hata hivyo, hili linakuwa na ukakasi hasa ikizingatiwa kuwa huwa wengi wana tabia ya kuwasifia marehemu badala ya kuelezea ukweli wa namna walivyoishi.

Kwa ujumla, Hamad alikuwa mwanasiasa mtatanishi ambaye aliweka mbele maslahi yake kuliko kitu chochote. Hatusemi hili kwa ubaya dhidi ya marehemu. Kama si Hamad, Zanzibar na hata Tanzania, zisingekumbwa na misukosuko zilizopitia hasa machafuko yaliyosababisha mauaji ya baadhi ya watu Visiwani kiasi cha Tanzaniakwa mara ya kwanza katika historia ya uwepo wake kama taifa kuzalisha wakimbizi wakati ilizoea kuwa kimbilio la wakimbizi kutoka karibu majirani zake wote.

Tumalizie kwa kusema Hamad alikuwa si mwanasiasa wa kawaida. Unaweza kumwelezea utakavyo kutokana na ule upande wake uliouona. Na huo si mwisho wa kumjua Hamad.

**Lala Mahali Pema Peponi Maalim Seif Sharif Hamad.**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# TAKUKURU ifanye hili kwa waajiri



Na Joseph Kulangwa

**Zamani nchini kulikuwa na mifuko kadhaa ya aina hiyo, ambapo watumishi walikuwa na hiari ya kujiunga na mfuko walioona unafaa, lakini baadaye ikaonekana utitiri wa mifuko hauna tija, hivyo kubakiza miwili; PSSSF kwa watumishi wa umma na NSSF kwa wafanyakazi wa sekta binafsi.**

FAINALI uzeeni. Ni maneno mawili maarufu sana katika jamii. Hutumiwa kuasa vijana wanapokuwa bado na nguvu, kuwahimiza kujibidiisha kufanya kazi na kujiandaa kwa maisha ya baadaye.

Mara nyingi huambiwa kujiwekea akiba ambayo itawasaidia pale watakapokuwa wamezeeka na kuishiwa nguvu za uzalishaji mali, hivyo kutumia akiba zao kama mbadala wa nguvu hizo.

Serikali nayo kwa upande wake, imekuwa na utaratibu ambao watumishi wa sekta zote, rasmi na isiyo rasmi, wanawekewa akiba zao kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii, ili wamalizapo muda wao wa kazi, kwa kuachishwa, kustaafu au kupata madhila mengine, basi fedha zao ziwasaidie.

Utaratibu huo umekuwa ukiwezesha mfanyakazi kukatwa kiasi kwenye mishahara yake na kiasi kingine kuongezwa na mwajiri, na kuhifadhiwa na mifuko hiyo, kwa mustakabali wa maisha ya watumishi hao.

Mifuko hiyo nayo kwa upande wao, imekuwa ikizitumia fedha hizo kuendesha miradi ambayo imekuwa ikichangia maendeleo ya nchi, huku michango ya watumishi ikibaki bila kutibuliwa na hatimaye mhusika kupokea fedha zake na faida kidogo.

Zamani nchini kulikuwa na mifuko kadhaa ya aina hiyo, ambapo watumishi walikuwa na hiari ya kujiunga na mfuko walioona unafaa, lakini baadaye ikaonekana utitiri wa mifuko hauna tija, hivyo kubakiza miwili; PSSSF kwa watumishi wa umma na NSSF kwa wafanyakazi wa sekta binafsi.

Hili lilikuwa wazo la msingi na lenye umuhimu mkubwa, kwa maisha ya baadaye ya mtumishi mstaafu au aliyeondoka kwenye utumishi kwa sababu yoyote ile, ikitazamiwa kuwa mara tu ajira inapokoma, mtumishi anapata haki yake sawia.

Hata hivyo, ulivyokuwa utaratibu, ni kwamba baada ya ajira kukoma, ilibidi mtumishi akae takriban miezi sita mpaka kupokea stahiki yake hiyo. Ulikuwa muda mrefu lakini hatimaye haki ilitendeka.

Hivi sasa kuna malalamiko kwa baadhi ya watumishi waliokoma ajira kwa sababu hizo hapo juu, kucheleweshewa malipo yao, ama kwa uzembe wa watumishi wa mifuko husika au kwa taasisi au waajiri kutopeleka michango kwenye mifuko.

Waliokuwa watumishi wengi wamekuwa mitaani wakifuatilia stahiki zao hizo bila mafanikio, huku wengine wakipoteza maisha na kuachia warithi kufuatilia lakini kwa usumbufu mkubwa.

Kibaya zaidi ni kwamba licha ya mifuko kujua nani hajawasilisha michango ya watumishi wake, hakuna hatua za makusudi na za wazi zinazochukuliwa kuwawajibisha ili wastaafu na wengine walipwe kilicho chao kwa wakati.

Hiyo inafanya watumishi hao kujisikia kama watu wasiotakiwa wanapokuwa hawako kazini na kuthaminiwa tu wanapokuwa kazini, na wengine hujikuta wamekumbwa na msongo wa mawazo na hata wanakumbwa na kiharusi au hata kupoteza maisha.

Inashindikana nini kwa mifuko kufuatilia waajiri hata kama ni kwa kufikishwa mahakamani na kuchukuliwa hatua, ili wenye haki yao waipate kwa wakati stahiki, badala ya kuzungushwa?

Kwa siku za karibuni, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imefanya kazi iliyotukuka ya kuokoa fedha za watu wengi waliodhulumiwa na hatimaye kupata haki hizo. Pengine ni wakati mwafaka sasa kwa taasisi hiyo, kupewa jukumu hilo la kufuatilia waajiri jeuri na kuwachukulia hatua ili Watanzania wanyonge walipwe mafao yao kwa wakati.

Ni kwa kufanya hivyo tu, ndipo serikali itakapokuwa imetenda haki kwa Watanzania na kutekeleza kaulimbiu yake ya Serikali ya Wanyonge inayotetea na kusaidia wanyonge.

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# JPM kuvunja jiji Dar amecheza kama Pele



Na Thobias Mwanakatwe

**Mwaka 1996 serikali iliivunja Halmashauri ya Jiji na kuunda Tume ya Jiji ambayo ilifanya kazi kwa miaka minne hadi mwaka mwaka 2000 serikali ilipounda mamlaka nne za serikali za mitaa za mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni jiji lenyewe na manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke.**

FEBRUARI 24, 2021 hakika itabaki kuwa historia kwa wakazi wa Mkoa wa Dar es Salaam na Watanzania kwa ujumla kutokana na uamuzi uliofanywa na Rais John Magufuli wa kutangaza kulivunja jiji la Dar es Salaam na kuipandisha hadhi Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kuwa jiji.

Wakati akitangaza uamuzi huo, alisema: "Nategemea kulivunja Jiji la Dar es Salaam, tunaweza kuifanya Ilala kuwa jiji lakini kuwa na madiwani wanakaa hapa juu, hawana miradi ya maendeleo wanakula posho na hawakuchaguliwa na watu hili nitalikataza. Manispaa moja ipandishwe hadhi kuwa jiji na zingine zibaki kuwa Manispaa."

Baada ya kutangazwa kwa uamuzi huo, mamia ya wananchi kupitia mitandao ya kijamii, wamepokea kwa furaha kwa sababu kimsingi jiji la Dar es Salaam lilikuwa mzigo tu na kuongeza matumizi kwa serikali.

Ukichimbua kwa undani unakuta kiutawala Jiji lilikuwa limegawanyika katika Halmashauri sita ambazo ni: Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na manispaa za Temeke, Ilala, Ubungo, Kinondoni na Kigamboni.

Sasa ukiangalia hapo juu kulikuwa kuna chombo tu kinaitwa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam lakini hakikuwa na eneo rasmi la kiutawala. Kwa maana nyingine, Halmashauri ya Jiji haikuwa ardhi inayoitawala, hivyo kutegemea vyanzo vya mapato kutoka halmashauri za manispaa.

Chombo hiki, yaani Halmashauri ya Jiji, kilikuwa na Meya wake na baraza lake huku kikiwa hakina vyanzo vya mapato, lakini kilitenga bajeti. Swali linakuja unapewaje bajeti huku miradi inahudumiwa na manispaa zenyewe?

Kwa mtazamo wangu, jambo hili lilichelewa. Lilipaswa kufanyika muda mrefu kwa sababu kwa miaka mingi mamilioni ya posho yameliwa na wajumbe waliokuwa wakikutana kwenye vikao vya jiji.

Kwa wasiofahamu historia ni kwamba Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imekuwapo tangu mwaka 1961 mpaka 1972 ambapo serikali ilizivunja halmashauri zote nchini na kuwa chini ya usimamizi wa serikali kuu (madaraka mikoani).

Serikali ilizirudisha Serikali za Mitaa, chini ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) na. 8 ya mwaka 1982 ambapo Halmashauri ya Jiji ilianza kutekeleza majukumu yake ya kutoa huduma kwa wananchi kuanzia mwaka 1983.

Mwaka 1996 serikali iliivunja Halmashauri ya Jiji na kuunda Tume ya Jiji ambayo ilifanya kazi kwa miaka minne hadi mwaka mwaka 2000 serikali ilipounda mamlaka nne za serikali za mitaa za mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni jiji lenyewe na manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke.

Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam lilikuwa linaundwa na madiwani 26 kutoka manispaa tano. Pia iliundwa na kupewa majukumu ya kuratibu na kusimamia shughuli za uendelezaji wa jiji.

Majukumu hayo ni kuratibu mamlaka na wajibu wa kila halmashauri za manispaa juu ya miundombinu na matumizi bora ya ardhi; kuandaa mpango mkakati kwa ajili ya kuhakikisha kuwa panakuwapo na maendeleo endelevu ya jiji; na kukuza ushirikiano kati ya mamlaka za malmashauri zote katika Jiji la Dar es Salaam.

Mengine ni kushughulikia masula yote yanayohusu ushirikiano kati ya mamlaka za serikali za mitaa zilizopo katika Jiji la Dar es Salaam; kuhakikisha panakuwapo amani na utulivu pamoja na kutoa msaada katika huduma kama vile Zimamaoto na maokozi, polisi na magari ya kubeba wagonjwa; na kutekeleza majukumu mengine yoyote kama itakavyokubalika na halmashauri zingine zilizopo.

Kadhalika kutekeleza majukumu ya itifaki na sherehe za kimkoa au /na kitaifa; uboreshaji wa muundo wa jiji kuwa mamlaka sita umeleta ufanisi mkubwa katika utoaji bora wa huduma kwa jamii kwani madaraka yamesogezwa karibu zaidi na wananchi.

Nimalizie kwa kusema hongera sana Rais umeweka historia mpya katika jambo hili. Bila shaka utawekwa kwenye vitabu vya kumbukumbu.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2015@gmail.com**

## DARASA LA NDOA

# Namna ya kukabili huzui ya kuondokewa na mtu wa karibu



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

**Wataalamu wa tiba wanasema mtu anapofiwa na mpendwa wake, mwili unazalisha kwa wingi kemikali ziitwazo "narcotic" ambazo huondoa uchungu. Mwili wa mwanadamu ni mashine inayojikarabati. Mtu anapolia, kemikali hizi hutolewa kwa njia ya machozi. Ndiyo maana ni muhimu kumwacha mtu alie ili atoe machungu aliyonayo katika nafsi.**

SUALA la kuondokewa na mtu uliyempenda na kumtegemea husababisha huzuni. Huzuni hii isiposhughulikiwa mapema, inaweza kusababisha matatizo makubwa ya kiafya na kisaikolojia kwa mtu kama vile shinikizo la damu, maumivu ya kichwa, kiharusi, magonjwa ya akili, kisukari, kukosa usingizi, kupoteza fahamu, kupoteza hamu ya chakula, mwili kudhoofu hata kusababisha kifo.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba akili inakuwa imekataa kukubali kuondokewa. Maswali mengi yasiyo na majibu, mifadhaiko na hali ya kukata tamaa hujitokeza.

Kutokana na uzito wa kuondokewa, ni muhimu kujua namna ya kukabili huzuni ili kuepuka athari zake na gharama zisizo za lazima. Mada hii imejikita zaidi katika huzuni itokanayo na kuondokewa na mtoto, mwenzi au mzazi kwa njia ya kifo katika familia.

Ni ukweli usiopingika kwamba, vifo hivi hugusa sana hisia za wanafamilia wengi. Ni kwa mantiki hii huwa ni jambo gumu na mtihani mzito kwa mwanandoa kusema kwaheri kwa mpendwa wake aliyeaga dunia.

Mwanadamu aliyezaliwa, iko siku atakufa. Pamoja na kutambua ukweli huu, hakuna mtu anayetamani kufa au kufiwa, labda mtu aliye na matatizo ya akili au mchawi.

Katika nyakati hizi, tunashuhudia vifo vya wale tuliowafahamu na ambao hatukuwafahamu. Kwa kuzingatia ukweli kuwa uhai wa mtu ukiondoka hauwezi kurejeshwa, Larry YEAGLEY katika kitabu chake kiitwacho "Grief Recovery" (a-c) na mwandishi wa makala hii (d-e), wanapendekeza hatua tano zinazoweza kumsaidia mtu kukabili huzuni ya kuondokewa kama ifuatavyo:

**FIKIRI**

Usizuie kufikiri. Kumbukumbu kuhusu marehemu na matukio wakati mlipokuwa pamoja lazima humjia mfiwa. Usiogope fikra zinapokujia. Acha fikra zikujie.Kufikiri ni mchakato ambao humuwezesha mfiwa kukubali kuondokewa.

Zungumza

Zungumza na watu ambao wako tayari kukusikiliza na si wanaokuhukumu. Usisite kuzungumzia tukio lilivyokuwa kwani husaidia kuondoa machungu. Kuzungumza ni mchakato ambao polepole hupunguza maumivu makali ya kuondokewa.

**LIA**

Kulia ni nafuu tuliyozawadiwa na Mungu wakati mtu anapokuwa katika hali ya mafadhaiko. Usizue kulia. Usizuie machozi bali lia na acha machozi yatoke vya kutosha. Machozi ni dawa ya uponyaji wa nafsi. Kulia ni sehemu ya kuachilia hisia za ndani.

Wataalamu wa tiba wanasema mtu anapofiwa na mpendwa wake, mwili unazalisha kwa wingi kemikali ziitwazo "narcotic" ambazo huondoa uchungu. Mwili wa mwanadamu ni mashine inayojikarabati. Mtu anapolia, kemikali hizi hutolewa kwa njia ya machozi. Ndiyo maana ni muhimu kumwacha mtu alie ili atoe machungu aliyonayo katika nafsi.

Kwa mantiki hiyo, kulia ni tiba bora sana kuliko vidonge vya usingizi pale mtu anapokuwa ameelemewa na huzuni ya kuondokewa. Kadiri siku zinavyokwenda, kemikali hizi hupungua kwa kuwa machungu nayo huwa yamepungua.

**CHANGAMANA NA WATU**

Ndugu na marafiki ni watu muhimu wakati wa huzuni ya kuondokewa. Kama kuna kipindi kigumu kwa mfiwa yeyote, ni kipindi baada ya mazishi, ambapo waombolezaji wanakuwa wameondoka na mfiwa kubaki peke yake. Hapa ndipo mfiwa anapohitaji sana watu wa kumtembelea ili kumchangamsha, kumfariji na kumtia moyo. Hata hivyo, watu wa kukutembelea wanapokosekana, usijifungie sana ndani, toka na changamana na watu wema.

**JISHUGHULISHE**

Ni muhimu mfiwa afanye shughuli mbalimbali za kuushughulisha mwili baada ya muda wa maombolezo kumalizika, kwani lazima maisha yaendelee baada ya kuondokewa. Katika kufanya shughuli mbalimbali, akili inajielekeza katika shughuli hizo zaidi kuliko msiba, hivyo, kusaidia kuondoa huzuni na majonzi pole pole.

Kufiwa ni hali ya kuhuzunisha. Ni hali yenye kuleta athari za kiafya na kisaikolojia pale mfiwa anaposhindwa kukubali huzuni; anapokosa faraja na watu wa kumtia moyo. Huzuni ya kuondokewa haitatuliki kwa haraka. Ni mchakato wa polepole.

Huzuni ya kuondokewa huweza kudumu ndani ya mtu kwa kipindi cha kati ya miezi sita hadi miaka miwili au mitatu kutegemeana na mazingira au aina ya kifo. Ni kwa msingi huu, mfiwa huhitaji ushauri nasihi ili kumsaidia kukubali hali iliyojitokeza.

Pamoja na kuondokewa, ni muhimu mfiwa amshukuru Mungu. Kushukuru ni tendo ambalo hufuata baada ya mtu kukubali na kupokea kilichotokea. Mawazo ya shukrani huleta uponyaji wa fikra. Kushukuru ni dalili ya ukomavu wa kiimani.

Mshukuru Mungu kwa umri na maisha ya pamoja Mungu aliyowajalia, kwa zawadi ya uhai wake kabla ya kifo kutokea, kwa mengi mliyoyafanya pamoja wakati wa uhai wake, na kwa mema mliyoyapokea kutoka kwake wakati wa uhai wake.

**LIPO TUMAINI**

Pamoja na kuondokewa, bado lipo tumaini kwamba, Mungu ni upendo kwako na anakuwazia mema siku zote. Jambo la msingi ni wewe kudumisha mahusiano mema na Mungu, kwani yeye ndiye mpaji, tulizo lako la kweli, na mponyaji wa kudumu wa nafsi iliyojeruhiwa na kuumizwa. Kwa hiyo, usimwazie Mungu kwa ubaya, kwani kuondokewa hakuondoi mamlaka, nafasi na ukuu wake katika maisha yako.

Ng'ang'ana na Mungu ili akusaidie kuzikabili changamoto za kuondokewa na kuwa na maisha yenye utulivu na mafanikio.

- **Dk. Mlyuka ni mchungaji wa KKKT na Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maoni, mafunzo na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au WhatsApp +255655865555.**

# MAISHA

FEBRUARI 28, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 10

## Kweli tunawatakia mema mabinti?



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Mambo muhimu ya kufahamu kabla ya kuuza nyumba yako



## HARUSI

Ukurasa 12



## UREMBO WA KUCHA

# Utunzaji asilia una faida nyingi

Ukurasa 14

# Kweli tunawatakia mema mabinti?

**Na Moses Ismail**



NI familia yenye mabinti wawili na kijana mmoja mvulana. Wanaishi na wazazi wao, baba na mama wanaowapenda kwa kiwango cha hali ya juu sana na ni wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Wawili, mvulana ambaye ni mtoto wa pili na msichana mkubwa mtoto wa kwanza wanasoma shule ya sekondari huku mdogo wao, msichana, yeye anasoma shule ya msingi darasa la saba sasa.

Mara nyingi mama yao anapoongea nao, katika maongezi yao jikoni, huwa akiwanasihi madada hao wawili kujiepusha sana na masuala ya wanaume, anawaambia: "Mkipata ujauzito mtafukuzwa shule na baba yenu atawafukuza hapa nyumbani."

Ndiyo, hakuna mama 'kichaa' anayeweza kuwaacha wanae wenye umri huu wa kupevuka bila ya kuwahusia juu ya mustakabali wao wa kimaisha iwapo watajiingiza katika masuala ya mapenzi wakiwa shuleni. Hakuna.

Wakati mama anakitoa nasaha kwa binti zake, baba yeye hana muda kabisa ya kuzungumza na kijana wake, mvulana, na kuweleza juu ya madhara ya kuwa na uhusiano na binti za watu. Hajawahi kuzungumza naye.

Zaidi amekuwa akimwambia mke wake, mama, kuwa azungumze sana na wanae juu ya masuala ya mahusiano na wavula, anamwambia: "Wasije wakatutia aibu kwa kutuletea 'mimba'. Nakuapia nitaua mtu nakuambia."

Lakini wakati wazazi hao wawili wakitumia nasaha na maneno ya vitisho hivyo baina yao kuhusu jambo hilo, la mabinti zao kutiwa ujauzito, wakati huo huo wanaona fahari kwa kijana wao mvulana. Wanamsifu kuwa ni kidume hasa.

Wanajua kuwa yule rafiki wa binti yao, anayekuja nyumbani kwao kila siku jioni na siku za Jumamosi na Jumapili, ni 'mchumba' wa kijana wao na uchumba huo umeunganishwa na dada yake. 'Wanafurahiaje'?

Mama alipojua hilo, alimweleza baba; "kidume chetu kimekamilikaa, kina mpenzi sasa", na baba alipomjua 'mpenzi' huyo, akawa anahakikisha kuwa kila anapo 'watembelea' basi hakosi chipsi na soda. Eti wanamkarim!

Wakati wazazi hawa wakilifurahia hilo, wanaamini kabisa kuwa eti binti yao atabaki salama, hawezi kuwa kama rafiki yake, 'mkwe wao', wanajidanganya kuwa binti yao bado hajajiingiza katika msaula hayo kabisa.

Ukweli ni kuwa ndege wenye mbawa zinazofanana huruka pamoja, kama wanavyo muona rafiki wa binti yao mkwe, na binti yao naye ni mkwe wa familia nyingine. Ndio, anapokelewa na kufanyiwa tafirija kama mwenzie.

Kimsingi ni kwamba kama tunawapenda mabinti zetu, tumeamua kuwalinda na janga la ujauzito wa utotoni, ni lazima wazazi wote tuhakikishe kuwa tunapinga binti ye yote kuwa na mahusiano na vijana wetu kwa kuishi na msemo huu; "binti wa mwenzio ni binti yako pia, umlinde."

## NA HAMIS KIDAGO 0657 207168 QUIZ

Andikakitenzi **Ouvrir** (yaani kufungua) katika nyakati tofauti kama zilivyoainishwa hapo chini.

**Indicatif**
**présent**
j' ……………
tu ……………
il/elle ……………
nous……………
vous ……………
ils/elles ……………

**imparfait**
j' ……………………
tu ……………………
il/elle ……………………
nous ……………………
vous ……………………
ils/elles ……………………

**future simple**
j' ……………………
tu ……………………
il/elle ……………………
nous ……………………
vous ……………………
ils/elles ……………………

**passé simple**
j' ……………………
tu ……………………
il/elle ……………………
nous ……………………
vous ……………………
ils/elles ……………………

**passé compose**
j' ai ……………………………
tu as ……………………………
il/elle a ……………………………
nousavons ……………………………
vousavez ……………………………
ils/ellesont ……………………………

**plus – que – parfait**
j' ………ouvert
tu ………ouvert
il/elle ………ouvert
nous………ouvert
vous……..ouvert
ils/elles……….ouvert

**futurantérieur**
j' ……….ouvert
tu ……….ouvert
il/elle ……….ouvert
nous ………….ouvert
vous ……….ouvert
ils/elles ………….ouvert

**passéantérieur**
j' eus
…………..
tueus ………….
il/elleeut ………….
nouseûmes ………….
vouseûtes ………….
ils/elleseurent ………….

**Conditionnel**
**présent**
j' …………….
tu …………….
il/elle …………….
nous …………….
vous …………….
ils/elles …………….


passé
j' aurais
………………
tuaurais ………………
il/elleaurait ………………
nousaurions ………………
vousauriez ………………
ils/ellesauraient ………………

**Infinitif**
**présent** **passé**
………. ………………….

Participe
présent passé
……………. ………./….
…………/tes
ayant ………………

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

JAMAA mmoja alipeleka redio yake kwa fundi, mara ilipofunguliwa kwa ajili kuanza kutengenezwa, ghafla walitoka mende wengi na kukimbia. Baada ya kuona hivyo Yule jamaa alimwambia fundi "Kamata hao watangasaji wanaisia huko"

**SWALI**
Ziwa Nyasa linapatikana upande gani wa Tanzania

# MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



## Uliwahi kujiuliza kwa nini watu wanaishi maisha wasiyoyapenda?

KARIBU tena msomaji wangu katika mwendelezo wa makala za Maisha Ndivyo Yalivyo. Leo tuangalie eneo ambalo limewafumba macho watu wengi wasijitambue.

Miaka ya nyuma niliwahi kujiuliza hivi ni kwanini nilikuwa naishi maisha yale niliyokuwa nayaona mbele yangu. Sikupata jibu zaidi ya kuridhika kuwa pengine maisha yangu ndivyo yalivyo.

Lakini leo nimefunguka, nagundua siri kwamba watu wengi wanaishi maisha wasiyoyapenda, maisha feki (si halisi) ambayo hawastahili. Wako watu, kwa mfano, ni wagonjwa lakini hawajui wataponaje, wengine wanashikiliwa na nguvu za giza (ushirikina), nguvu za mizimu na hawajui wanajinasuaje.

Wanasumbuliwa na matatizo yanayojirudiarudia. Kila mwezi anaugua mwanafamilia, kila mwaka anakufa mtu kwao au kila ifikapo tarehe fulani kinatokea kitu kibaya kwenye familia.

Ukiona yote hayo yanatokea, elewa kuwa iko siri iliyojificha na ni muhimu ujue jinsi ya kutoka kwenye tatizo hilo. Lipo neno moja la Kigiriki ambalo nitalielezea kiroho ili ujue lina uhusiano gani na mambo ya kiroho. Na pia neno hilo lina uhusiano gani na mtu anayeishi maisha asiyoyaelewa.

Neno hilo ni 'FANTAS MAGORIAN'. Hili ni neno la Kigiriki, linapatikana kwenye Google. Lina maana kadhaa ikiwamo ile hali ya kuishi kwa kile kitu ambacho umekiona kwenye ndoto. Yaani ile hali ya wewe kuota ndoto mbaya.

Watu wengi hawaelewi kuwa kuota ndoto mbaya hakuishii kuiota ndoto hiyo, bali unaanza kuishi maisha ya ile ndoto mbaya uliyoiota. Yaani ile ndoto mbaya inaanza kutokea. Mambo mengi yanayowatokea watu katika ulimwengu wa damu na nyama(unaoonekana), tayari yalianza kuwatokea kwenye ndoto(Ulimwengu usioonekana kwa macho ya kawaida).

Utaona mtu anashangaa kwamba kile alichokiota kinaanza kutokea. Sasa ukianza kuona ndoto mbaya unazoziota zinaanza kutokea, ujue hiyo ni Fantas Magorian.

Maana nyingine ya Fantas Magorian, ni kuishi vile wanavyotaka maadui zako. Yaani unaishi sawasawa na maadui zako. Kama ni mlevi, mzinzi atahakikisha unaishi maisha kama yake. Maandiko ya Mungu yanasema, adui wa mtu ni wa nyumbani mwake. Ni rafiki hana mafanikio atang'ang'ana ufanane naye.

Huyataki maisha hayo, lakini unalazimika kuyaishi. Bibi ni mchawi anakufundisha uchawi. Bibi anataka mjukuu awe mwenyekiti wa wachawi ijapokuwa hapendi, bibi ndiye anayemuamulia.

Yuko mtu mmoja nilimkuta kwenye lindo(mlinzi), nilipomuuliza taaluma yake akasema ni mwanasheria lakini hapati kazi. Yawezekana amefungwa na roho za kichawi au mizimu ya kwao. Au laana, maneno yaliyotamkwa kwamba hatafanikiwa.

Katika mazingira kama hayo ni muhimu sana kukataa kuishi kama maadui zako watakavyo. Ni lazima ufaye maombi ya kumsihi Mungu afichue maadui zako waliojificha. Mungu anapenda watu waishi maisha ya ndoto zao, siyo ya kulazimishwa na maadui.

Maana nyingine ya Fantas Magorian ni kusababishiwa vitu feki katika ulimwengu wa roho. Wapo watu leo wanaishi maisha feki (siyo halisi). Walishakufanyia 'fojari''. Unaota ndoto majina kwenye kitambulisho au hati ya kusafiria(pasipoti) ni yako lakini picha siyo yako.

Unaweza kutengenezewa sura feki. Unajiona uko sawa kumbe usoni umevishwa kinyago. Ndiyo maana watu wanakuogopa, hawakupendi. Umefunikwa usoni, ila hujui. Watu hawakuoni, ukiomba kazi hupati, mchumba hupati. Wachawi wana maengo yao hutengeneza vitu feki.

Unaweza kuoa mke ukaamini kuwa umepata kisura, baada ya muda anabadilishwa na maadui, unamuona kituko. Yale yaliyokuwa yanakuvutia kwake kabla, sasa hayapo, ni kero juu ya kero. Tayari ni maisha feki ya ndoa, hakuna raha wala amani.

Maisha feki yanaweza pia kusababishwa na laana iliyowahi kutamkwa na mababu au mabibi zetu. Ulipaswa kuwa na maisha mazuri aliyokusudia Mwenyezi Mungu, lakini sasa laana ndiyo inayokutesa.

Lazima tufichue kilichojificha kwenye ulimwengu wa roho ili tujinasue na maisha feki ambayo watu wengi wanaishi leo. Tukatae feki za shetani. Maisha Ndivyo Yalivyo.

Wapo watu wameridhika na maisha waliyo nayo au kiwango walicho nacho. Kumbe hilo siyo kusudi la Mungu bali mpango wa shetani kukupiga upofu.

***Bila shaka msomaji wangu umejifunza jambo hapo. Niishie hapa ukiwa na maoni au kisa cha kimaisha tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

# NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



## Elimu ya kanuni za VICOBA iwafikie wananchi kwa wingi

ULE mwongozo wa usimamizi wa vikundi vidogo vya huduma za kifedha uliosubiriwa kwa muda mrefu, sasa uko wazi, ikiwamo kanuni za sheria ya huduma ndogo za kifedha ambayo inaweka bayana mambo ya msingi yanayopaswa kufanyika.

Kabla ya kutolewa kwa taarifa hizo, kulikuwa na taarifa nyingi zilizozua taharuki kwa wananchi walio kwenye vikundi kiasi cha baadhi kusambaratika na kugawana fedha alizokuwa amehifadhi.

Baadhi walitozwa fedha za usajili ngazi ya serikali za mitaa jambo ambalo halikutakiwa kufanyika hivyo, bali kusajili bure kwa kuhakikisha vikundi hivyo vinakuwa endelevu.

Tayari Benki Kuu ya Tanzania (BoT), imeeleza kuwa hakuna tozo wala ada, bali kilichocheleweshwa ni kutengeneza mifumo itakayotumika kusajili vikundi hivyo.

Lengo ni kuvitambua vikundi, viongozi, katiba na viongozi wao ikiwamo taarifa za mikopo kwa wanachama, jambo ambalo litapunguza mikopo chechefu kwa kuwa sasa itakuwa ni rahisi kupata taarifa na mienendo ya wakopaji.

Kazi kubwa kwa sasa ni kwa maofisa maendeleo ya jamii kutumia mfumo kusajili vikundi katika maeneo yao, ambao wataalam wa BoT wanasema ni ndani ya saa mbili na siku 14 kikundi kinapata cheti cha usajili.

Hizi ni habari njema sana ambazo sasa zinasubiri utekelezaji kwa kuwa vikundi vingi vimeshindwa kusajiliwa na kupata cheti kutokana na kukosekana kwa taarifa sahihi ambazo sasa ziko wazi.

Naamini sasa maofisa maendeleo ya jamii watafanyakazi hiyo kwa weledi na kutokuwa sehemu ya usumbufu au mwanya wa kudai rushwa kwa wananchi.

Tunaamini hakutakuwa na usumbufu kwamba viongozi wa vikundi wanatumia gharama kusafiri kwenda makao makuu ya halmashauri au manispaa halafu vinakosa huduma kwa madai kuwa mfumo haufanyi kazi au kuna rushwa inatakiwa kutolewa.

Uko usumbufu ambao huanzia serikali za mitaa wanapoona ni kikundi yanatengenezwa mazingira ya kupata fedha kutoka kwao ili kupata barua ya utambulisho, na wanapofika manispaa wanatozwa fedha ndiyo wapat usajili.

Ikiwa utaratibu huu utafanyika kwa ufanisi ni wazi kuwa vikundi vingi vitajitokeza kusajiliwa, lakini kukiwa na mazingira ya kugeuza vikundi mtaji ni wazi kuwa vingi vitakimbia na kuanza kuficha fedha nyumbani.

Moja ya matakwa ya kikanuni ni kikundi kuwa na akaunti benki na lazima vikundi viwe na jina moja la kuvitambulisha kama kikundi kidogo cha huduma za fedha.

Muhimu jambo hili likasimamiwa kwa ufanisi mkubwa ili kuvisaidia vikundi kujisajili na kufahamika, na matarajio ya wengi itaondoa au kumaliza utapeli au dhuluma zilizofanywa na baadhi ya watu kuchukua fedha za kikundi na kutokomea.

Zimebaki siku 30 za vikundi kusajiliwa matumaini yangu ni kuwa vyote vitafikiwa na elimu sahihi ili wafanye maamuzi sahihi ya kutekeleza wajibu wa kisheria, na hilo litafanikiwa iwapo madiwani wataelimishwa ipasavyo na kupekeka elimu hiyo ngazi ya kata, vijiji, vitongoji na mitaa.

Ni muhimu utoaji elimu ukanda sambamba na maofisa maendeleo kuhudhuria vikao vya maendeleo ya kata (WDC) ambavyo Mwenyekiti wake ni Diwani, Katibu Mtendaji kata na wajumbe ni wenyeviti wa vijiji ili kuelimisha na kisha elimu hiyo kusambaa.

Lakini ni muhimu sana kanuni zikasambazwa kwenye mitaa, vitongoji na vijiji kwa muundo wa vipeperushi ili wananchi wasome na kuelewa kilichomo na wasizolewe na elimu siyo sahihi ambayo itawapoteza.

Naamini elimu ikitolewa ipasavyo hakuna kikundi kitaachwa nyuma, na ikiwa vikisajiliwa vyote maana yake hata usalama wa fedha za wananchi utakuwa ni mkubwa kwa kuwa sasa watatoka kuweka fedha nyumbai kwa mtu bali benki ambako ni salama, na isitoshe itawezesha fedha kuwapo kwenye mzunguko wa uchumi, kukopesha wengi na kuendesha shughuli za kiuchumi.

Kukiwa na vipeperushi vya kanuni hizi kutasidia wengi kujua kilichopo na kupunguza taarifa za uongo ambazo zilishasambaa na kuwaogopesha wengi na kurudi enzi za kuhifadhi fedha kwenye vibubu.

Haitarajiwi kuwapo kwa malalamiko, lakini tunatarajia mamlaka nyingine za serikali zitakuwa macho kufuatilia suala hili kwa karibu, ili ule utaratibu wa kutoza fedha wananchi kwa huduma ambazo ni bure uishe ili wapate huduma muhimu kama inavyotakiwa katika ofisi za umma.

***Mungu ibariki Tanzania***

# HARUSI











Ilikuwa ni usiku wa furaha kwa familia ya Dokas Stuati, katika sherehe ya kumuaga binti yao iliyofanyika Februari 14, mwaka huu kwenye ukumbi wa sekondari ya Usagara, mkoani Tanga.



MITINDO

# Wikiendi yako katu haichoshi



SIKU ya mwisho wa wiki inakuwa maalum kwa watu mbalimbali kujumuika pamoja ikiwa katika familia, marafiki au jamaa wa karibu kwa ajili ya kupeana furaha.

Wapo wanaokwenda fukwe za bahari, kumbi za burudani na maeneo ya uuzaji wa vyakula vitamu.

Hata hivyo inakuwa tabu kukamilisha siku hiyo kama mtu hajui nini afanye ili awe tofauti na siku zingine katika kimavazi, kimapambo na hata muonekano wake. Hata hivyo, unaweza kufanya mambo haya na kubadilisha mwonekano wako ghafla na kuwa vizuri zaidi.

Njia za haraka ambazo wataalamu wa masuala ya mavazi wanashauri kuzifuata wakati unataka kutoka lakini hujajiandaa vizuri ni kama zifuatazo.

**NYWELE**

Kama wewe ni mwanawake una nywele nyingi, unashauriwa kuzitengeneza katika mitindo ya kuning'inia, kuzibana au kuzifunga kwa skafu. Watu wenye nywele fupi wanashauriwa kuzichana vizuri na kupaka mafuta ya kung'arisha.

Wataalamu wanasema kuziachia nywele ndefu katika mfumo wa kulala nyuma zinamfanya mtu kuwa na mwendo mzuri.

Weka mapambo kwenye nywele zako, wengi wanaweka vibanio vyenye nakshi za kuvutia, lakini hilo halitoshi kwani unaweza kufunga kitambaa juu ya nywele au kuvaa hijab ili kuficha nywele.

**MKUFU**

Baada ya kuhakikisha umeweka nywele zako vizuri, vaa mkufu wa aina yoyote shingoni.

**MAVAZI**

Chukua nguo uliyohifadhi vizuri ndani ya kabati au kwenye enga na kasha vaa. Unatakiwa kuchagua nguo zenye rangi za kung'aa kwani siku ya mwisho wa wiki unatakiwa kuonekana zaidi.

5. Baada ya matayarisho hayo, weka vipodozi vichache kwenye uso wako.Inashauriwa ukiwa na muonekano wa asili ni vizuri zaidi na endapo utahitaji kuongeza basi weka vipodozi visivyochosha uso.

## UREMBO



## UREMBO WA KUCHA



# Utunzaji asilia una faida nyingi

WENGI wetu ukimbilia katika saluni maalum kwa ajili ya kuziosha na kuzipendezesha kucha.

Licha ya kuwa na imani kuwa saluni ni sehemu nzuri ya kuzitengeneza kucha, lakini si sehemu salama kwa ajili ya afya ya mwili kwa hivi sasa.

Kutokana na uwepo wa tahadhari, hata wewe mwenyewe unaweza kuzitunza na kuziboresha kucha zako ukiwa nyumbani.

Hata hivyo, unatakiwa kujipangia na kuzingatia mlo mzuri, usafi na matunzo sahihi ya kucha zako

Ukiwa na utaratibu huu utaweza kulinda matumizi ya pesa na kukuepusha kuzidisha kemikali zinazo tumikakwenye vifaa vya kucha Zifuatazo ni dondoo zitakazokusaidia kutunza kucha zako katika njia halisi.

Matumizi ya mafuta

Ukiwa unajipaka mafuta au losheni mikononi, pitisha pia kwenye nyama za pembeni ya kucha.

Kama mikono imekauka unatakiwa kutumia 'sanitaizer' mara kwa mara , kwahiyo jitahidi sana kupakaa mafuta pale unapo maliza kujisafisha.

Mafuta ya nazi ni mazuri kwenye kucha.

**KUKATA KUCHA**

Epuka kukata nyama za pembeni ya kucha kwani inaweza kukupa madhara kwani nyama hizo zipo kwa ajili ya kinga ya ngozi yako na kuepushwa na magonjwa.

**EPUKA KUPAKA RANGI ZA KEMIKALI**

Rangi za kucha ubeba kemikali mbaya na wakati mwingine inaweza kukupa madhara, hivyo kabla ya kutumia jaribu kusoma maelekezo. Kuna kampuni nyingi hawaweki kemikali hizo, au unawea kununua rangi inayotumia maji.

**CHAGUA 'REMOVER' YENYE UASILIA**

Kama ukitaka kuondoa rangi, tafuta remover' ambayo imetengenezwa bila kemekali za sumu.

**JITENGEZEE TIBA ASILI YA KUCHA**

Muhimu kujua tiba asili ya kucha kama unataka kuziimarisha zaidi.

Kwa mfano vijiko viwili vidogo vya mafuta ya castor, vijiko viwili vidogo vya chumvi na kijiko kimoja cha mafuta ya ngano inatosha kabisa kung'arisha na kuondoa vijududu katika kucha.

## MAPISHI

**Na Mary Geofrey**

# Chapati za siagi na mtindi



CHAPATI ni aina ya chakula kinachopendwa na watu ka mlo kamili wa asubuhi au jioni.

Hata hivyo chakula hiki kinaweza kuliwa wakati wowote, lakini ili kiwe na ladha zaidi huambatana na maharage, rosti la nyama, maini, supu na chai au juisi.

Chapati hazipendezi zikiwa kavu kama kaukau, zitakiwa kuwa laini na hivyo unatakiwa kuwa makini.

Kuna aina mbalimbali za mapishi ya chapati za kusukuma ambazo ndizo ninazozizungumzia. Wengi tumezoea mapishi ya chapati za kukanda na maji tu lakini leo tunawabadilishia aina ya chapati na tunaelezea za kusukuma kwa kutumia maziwa mtindi na siagi.

**MAANDALIZI**

Mahitaji kwa ajili ya kupika chapati za kusukuma kwa kutumia maziwa mtindi na siagi ni unga wa ngano kilo moja, chumvi saizi na mafuta vijiko vitatu.

Andaa pia siagi vijiko vitatu, maji ya uvuguvugu glass mbili, maziwa mtindi glass moja na mayai mawili.

**JINSI YAKUCHAGANYA**

Mwanzo weka beseni mimina unga bakisha kidogo kwa ajili ya kusukumia wakati unataka kuzikaanga.

Mimina mtindi, mayai, mafuta, chumvi na siagi, anza kuchanganya unga hadi ubadilike rangi.

Anza kuweka maji ya uvuguvugu glass mbili, anza kukanda mpaka ulainike na ukiwa tayari uache kwa dakika 12. Baada ya dakika hizo kuisha anza kukata matonge saizi unayoitaka na kama unataka chapati kubwa unaweza kukata matonge 13 tu.

Anza kusukuma matonge yako kwa kutumia unga uliobakisha na nyunyuzia mafuta juu ili ziwe laini na kunja matonge kwa mara ya pili.

Ziache kwa nusu saa na anza kuzisikuma na kukaanga kwa kutumia frampeni na moto uwe kiasi ili zisiungue.

Chapati zako zitakuwa tayari kwa ajili ya kuliwa familia na aina ya mboga unayopendelea.

## MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**

# Mambo muhimu ya kufahamu kabla ya kuuza nyumba yako



BIASHARA ya nyumba na uwekezaji wa majengo ya kisasa inaendelea kushika kasi kila siku.

Lengo kuu la makala hii ni kupeana maarifa kuhusu mambo muhimu ya kuzingatia kabla ya kuuza nyumba kwa kujitathmini na kufanya uamuzi sahihi.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Mdoe Kimbe, anasema miongoni mwa mambo ya kuzingatia kabla ya kufikia uamuzi wa kuuza nyumba ni kutathmini lengo au sababu kuu ya kufanya hivyo.

Anasema wakati tulio nao biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo unafanyika kwa mbinu za kisasa ambazo ni matokeo chanya ya ukuaji wa sekta ya ujenzi inayotokana na mapinduzi ya teknolojia mbalimbali duniani.

"Watu binafsi, kampuni na taasisi nyingi zimejitokeza kwa wingi kuzitumia fursa zinazoendelea kujitokeza kila siku kwenye biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo hususani kwa kuiendesha kisasa zaidi kwa kutoa huduma za makazi na biashara kwa wadau mbalimbali,"anasema Kimbe na kuongeza:

"Lakini kuna baadhi ya watu wamejikuta wakiingia kwenye uuzaji wa majengo yao kutokana na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo kwenye maisha ndiyo maana ninashauri kwamba ni muhimu sana ukajitathmini kabla ya kuuza nyumba yako, je, ni kwa lengo la kibiashara au kutokana na kushindwa kukabiliana na msukosuko wa changamoto za maisha zinazokukabili."

"Kutulia na kujitathmini kutakusaidia ufikiri vizuri na wakati mwingine kuepuka majuto kama hukuwa na ulazima wa kuuza nyumba yako," anasisitiza.

Jambo lingine, anasema kabla ya kufanya uamuzi huo wa kuuza nyumba ni vema kutathmini bei na gharama ya mauzo ambayo unayapeleka sokoni ili kukusaidia kufahamu kiwango halisi na faida au mapato utakayopata kwa kutimiza malengo unayokusudia.

Mtaalamu huyo anashauri kwamba ni muhimu kuzingatia kwa kuhakikisha nyumba yako inakuwa na muonekano mzuri na kushawishi wanunuzi, na kwamba kama rangi yake ilikuwa imechakaa ni vema kuipaka upya pamoja na kuzingatia kuwa inakuwa safi wakati wote.

Anasema mvuto wa nyumba nao utakusaidia kukuongoza pia katika namna ya kufanya tathmini ya bei na itasaidia inunuliwe kwa muda mfupi.

Pia anashauri kwamba kabla ya kufanya uamuzi wa mauzo, ni vyema kutathmini hali ya soko la nyumba na si kukurupuka.





## MPANGILIO

# Dondoo ya kupamba chumba cha mtoto

**1:** Bandika makaratsi ya ukutani yenye michoro ya wanyama katika chumba cha kulala cha mtoto, kama ikiwa kuchora. Waache watoto wapate uamuzi na kuwaweka katika nafasi kuelezea kile wanachokiona ukutani.


**2:** Kama watoto wana umri mkubwa kiasi weka vitu vya kujifunzia kusoma na kuandika, meza ndogo na kiti cha kukalia kama akitaka kujisome.

**3:** Watoto wadogo wana fujo nyingi, hakikisha chumba kinakuwa hakina vitu vingi ili kuacha uwazi wa kucheza kirahisi.Hii inafanya kuwa rahisi kufikia sehemu moja hadi nyingine pamoja na kuona vitu vyake vya kuchezea bila matatizo.

**4:** Kama nafasi ni ndogo unatakiwa kuweka kitanda ukutani kabisa, hii itafanya kuwepo na nafasi kwa ajili ya kucheza.



# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2020
SMS - 0621 412 879
Nimekuja kuwashukuru na kuwaambia kwamba sijagombea ili NISHINDE ila KUNOGESHA
JUKWAANI
Majirani mnasubiri Nifulie Niuze kausafiri kangu mnicheke Eti kisa sitoi Lifti... "BADO SANAAAAAA!"
Sijui mke wangu kajuaje kama nina Mchepuko Bar.
Kwa hiyo unataka kusema kwamba "FRIJI LANGU HALIGANDISHI?"
Aaaaah wapi....Mbona Ulipobwagwa ulikwenda Kuamkia "AISIYUU?"
Baelezee
KERO yangu ni moja tu! Sijui kwa nini POMBE IMENIKONTROO kama Mpira na DARUGA!
Ule Wimbo wa Singeli wanaoimba "WANGA WABAYA" sasa ndio nauelewa
Sio wote wanye safari wengine wasindikizaji
"UNAJIKOSHA!"
Mimi ni hatari sana kwenye "MAHESABU"
Unahesabu nini wakati kila siku unasema HUNA HELA!
Alikuwa anajidai sana, tumemshikisha Adabu kwenye Boksi la Kura
Kilichomtupa ni kutokunywa nasi uji misibani
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...HATA AKIKUCHEKEA, MAUMIVU BADO UNAYO....

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda yakiri kulipa ndege iliyombeba Rusesabagina

**KIGALI,** RWANDA

RWANDA imekiri kuhusika na malipo ya ndege iliyomsafirisha mpinzani wa serikali, Paul Rusesabagina, kutoka Dubai hadi nchini humo mwaka jana

Akishiriki katika kipindi cha mahojiano katika televisheni ya Al Jazeera, Waziri wa Sheria wa Rwanda, Johnston Busingye, alikubali nchi hiyo ililipia gharama baada ya ushahidi wa video ambayo yeye na washauri walituma katika kituo hicho kimakosa.

Busingye alisema malipo yalilipwa baada ya kukamilika mpango wa kumkamata kwa usaidizi wa jasusi wa nchi hiyo ambaye alikuwa akifanya kazi na Rusesabagina.

"Kulikuwa na mtu aliyekuwa anafanya kazi na Rusesabagina kwa muda mrefu , ambaye alikuwa ni akifanya kazi na idara yetu ya upelelezi wa makosa ya uhalifu , alikubali kumlaghai na malipo yalitumiwa kwa jinsi gani Rusesabagina anaweza kuletwa Rwanda," aliongeza.

Busingye alisema serikali ya Rwanda ilitekeleza sheria wakati ilipomlaghai Rusesabagina, ambaye ana uraia wa Ubelgiji na Marekani, kupanda ndege iliyompeleka hadi Kigali.

Ni kwa jinsi gani mwanasiasa huyo wa upinzani alifika Rwanda bila utashi wake, ni mojawapo ya mambo yanayojadiliwa katka kesi inayomkabili.

Mwenyewe anadai alitekwa nyara na kufikishwa nchini humo bila ridhaa yake.

Hata hivyo, katika mazungumzo na waandishi wa habari mwezi Septemba mwaka jana, Rais Paul Kagame alisema alijileta mwenyewe.

Katika taarifa ya Wizara ya Sheria, ilipinga mazungumzo hayo na kueleza yalitokana na sauti ya siri iliyorekodiwa ambayo haielezei sera ya serikali.

Tarifa hiyo linasema kuwa msimamo wa serikali ni kwamba Rusesababigina alikamatwa kulingana na sheria na hakuna ukiukwaji wa haki ya mtuhumiwa huyo.

Katika mazungumzo na mwandishi wa habari wa Aljazeera Marc Lamont Hill, Bwana Busingye alisema:

Katika video iliyotumwa kwa Aljazeera kimakosa , Busingye alikubali kuwa wakuu wa gereza walinasa mazungumzo baina ya Rusesabagina na mawakili wake.

Akizungumza na washauri wake alisema kuna waraka mmoja ambao ulikuwa unaashiria kuwa alikuwa anataka kutoroka na barua hiyo ilikamatwa na wakuu wa gereza, lakini Rusesabagina alirudishiwa.

Al Jazeera ilisema kuwa katika mazungumzo ya awali iliyofanya na Busingye, alikuwa amekana kuwa wakuu wa gereza hawahusiki kusikiliza mazungumzo kati ya Rusesabagina na mawakili wake.

**BBC**



Mwanamume mmoja akiwaka moto wakati wa maandamano mbele ya ofisi ya Rais wa Ukraine zilizopo Kiev. Mtu huyo aliyetambulika kwa jina la Oleksandr Burlakov, aliokolewa na kueleza nia yake ilikuwa kutaka mamlaka juu ya kusikiliza shida yake ya umiliki ardhi. **(PICHA: REUTERS)**

## Amnesty yaituhumu Eritrea kuua raia Axum

**ADIS ABABA,** ETHIOPIA

SHIRIKA la kutetea haki za binadamu la Amnesty International, limevishutumu vikosi vya Eritrea kwa mauaji ya mamia ya raia katika eneo la Kaskazini mwa Ethiopia katika muda wa masaa 24 mwaka jana.

Mauaji hayo ambayo yametajwa kama uwezekano wa uhalifu dhidi ya ubinadamu, yamepingwa na serikali ya Eritrea.

Hata hivyo, shirika moja la kutetea haki za binadamu la serikali ya Ethiopia, pia limetoa taarifa ambayo ilielezea mauaji kama hayo japo kwa maelezo machache.

Ilikuwa ni hatua ya nadra ya kukiri rasmi kwa Ethiopia kwamba vikosi vya Eritrea vilishiriki katika mzozo uliotokea wakati wa msako wa serikali katika eneo la Tigray mwaka jana.

Waziri wa habari wa Eritrea, Yemane Meskel, alikataa ripoti hiyo ya amnesty na mara kwa mara alisema vikosi vya nchi yake havikushiriki katika mzozo huo

**DW**

# Marekani yamhusisha Mohammed Bin Salman mauaji ya Khashoggi

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imetoa ripoti yake ya kijasusi ambayo imebaini Mwanamfalme wa Saudia Arabia, Mohammed bin Salman, ndiye aliyeidhinisha mauaji ya mwandishi wa habari wa nchi hiyo Jamal Khashoggi mwaka 2018.

Ripoti ambayo iliidhinishwa kutolewa na Rais Joe Biden, ilisema mwanamfalme huyo aliidhinisha mpango wa kumkamata au kumuua Khashoggi.

Marekani ilitangaza vikwazo kwa Wasaudia ladhaa lakini si kwa mwanamfalme huyo.

Hata hivyo, Saudi Arabia ilipinga ripoti hiyo ikiitaja kuwa hasi, uongo na isiyokubalika .

Mwanamfalme Mohammed, ambaye anatambuliwa kama mtawala wa ufalme, amekanusha kuhusika kwa namna yoyote ile katika mauaji hayo.

Khashoggi aliuawa alipokuwa akiutembelea ubalozi mdogo mjini Instanbul , Uturuki , na mwili wake ulikatwakatwa.

Mwandishi huyo wa habari aliuawa akiwa na umri wa miaka 59, wakati mmoja aliwahi kuwa mshauri wa serikali ya Saudi Arabia na alikuwa karibu na utawala wa Ufalme , lakini alikosana nao na kwenda kuishi nchini Marekani mwaka 2017.

"Tunatathmini kwamba Mwanamfalme wa Saudi Arabia Muhammad bin Salman, aliidhinisha operesheni katika ubalozi wa Instanbul ya kumkamata au kumuua mwandishi wa habari wa Saudia, Jamal Khashoggi," ilisema ripoti hiyo kutoka ofisi ya mkurugenzi wa ujasusi wa taifa hilo.

Ripoti hiyo ya ujasusi inaonyesha sababu tatu za kuamini kwamba mwanamfalme lazima aliidhinisha operesheni hiyo.

Sababu hizo ni mwanamfalme huyo ndiye anadhibiti uchukuzi wa uamuzi katika ufalme tangu mwaka 2017. Uhusika wake wa moja kwa moja katika operesheni ya mmoja wa washauri wake pamoja na wajumbe wa kikosi cha ulinzi wa usalama wake na uungaji mkono wake wa matumizi ya ghasia kunyamazisha wapinzani walioko nje ya nchi.

Ripoti hiyo inayataja majina ya watu binafsi wanaodaiwa kushirikiana na kuhusika katika mauaji ya Khashoggi. Lakini ilisema hawakukufahamu mapema wale waliohusika kupanga na kumdhuru.

**BBC**

MAKALA

# Waraka wangu kwa Waziri wa Kilimo



Na Magabilo Masambu

**Nchi hii ina maeneo makubwa sana ambayo hayajatumika ipasavyo katika kilimo, angalau bahati hiyo tunayo lakini tunakwama wapi? Tuna maeneo yenye maji ya kudumu kama maziwa na mito tunayatumiaje katika kuzalisha chakula cha kutosha katika nchi?**

NDUGU Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda. Pole na hongera kwa ujenzi wa taifa. Nitumie nafasi hii kusema machache kuhusu wizara yako kama wizara mama ambayo nafikiri imebeba Watanzania wengi zaidi waliojiajiri na walioajiriwa kupitia kilimo.

Kilichonisukuma niandike waraka huu kwako ni juu ya hali halisi ya wakulima nchini. Inawezekana unafahamu zaidi kuliko mimi kuhusu changamoto wanazokutana nazo wakulima wa Tanzania. Lakini hilo halinizuii kutoa maoni yangu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 8(1), (2) lakini kama mtanzania mwenye nia njema kabisa na nchi yangu pamoja na watu wake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), muda si mrefu maeneo mbalimbali yatakuwa na mvua kiasi au nyingi. Tafasiri yake tunaelekea katika msimu wa kilimo. Nimejaribu kufanya utafiti mdogo tu juu ya gharama za pembejeo kwa maana ya mbegu, mbolea na dawa kwa ajili ya kuhudumia mashamba. Nimegundua kuwa bei za pembejeo ni kubwa mno kiasi cha kufanya wakulima wengi kushindwa kumdu gharama hizo.

Sekta ya kilimo inachochea maendeleo katika sekta zingine. Hatuwezi kuwa na viwanda bila kuwa na malighafi za kutosha. Hatuwezi kupunguza tatizo la ajira kama sekta ya kilimo haitakuwa kimbilio la wengi hasa vijana waliomaliza ngazi mbalimbali za kitaaluma.

Kubwa zaidi, hatuwezi kuona nafuu ya maisha kama hatutakuwa na chakula cha kutosha. Maana yake hali ya maisha itaendelea kuwa mbaya zaidi kama uzalishaji katika kilimo hautakuwa wenye uhakika.

Tumekuwa na kauli mbalimbali toka awamu ya kwanza kuhusu kilimo lakini nafikiri bado kuna tatizo kubwa katika mikakati inayochukuliwa ili kuboresha mazingira ya wakulima wakubwa na wadogo nchini.

Tulikuwa na kilimo ni uti wa mgongo, tukawa na kilimo kwanza,btukaja kilimo ni biashara nafikiri sasa tuna kilimo ni ajira. Swali kubwa hapa ni kwa namna gani kaulimbiu hizi zimesaidia kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo?

Nchi hii ina maeneo makubwa sana ambayo hayajatumika ipasavyo katika kilimo, angalau bahati hiyo tunayo lakini tunakwama wapi? Tuna maeneo yenye maji ya kudumu kama maziwa na mito tunayatumiaje katika kuzalisha chakula cha kutosha katika nchi?

Nataka nikuhakikishie Waziri kwamba fedha yetu itakuwa na thamani tu pale tutakapokuwa tumezalisha chakula cha kutosha nchini. Fedha kukosa thamani ni pamoja na kutumia fedha nyingi katika kununua vitu vichache.

Leo hii ukienda sokoni na Sh. 10,000 hata mfuko wa Sh. 500 haujai na fedha inakuwa imekwisha. Tafsiri yake ni kwamba vitu sokoni ni vichache hivyo lazima uhitaji uwe mkubwa kitu ambacho kinapandisha bei.

Ndugu Waziri, eneo la taaluma ya kilimo. Sasa hivi nchi hii walimu wa somo la kilimo ni wa kutafuta na tochi. Kwa maoni yangu wizara yako ishirikiane na wizara ya elimu kufanya mabadiliko ya haraka ili kupata walimu wengi wa somo la kilimo, ili somo la kilimo lisiwe la kuchagua (option). Kila anayemaliza elimu ya kidato cha nne awe na taaluma ya kilimo ili kuhakikisha wale watakaokuwa wanashindwa kuendelea na masomo wakiamua kufanya kilimo basi wafanye kilimo cha kisasa.

Kukosekana kwa chakula cha kutosha, kumesababisha upendo kwenye familia kupungua na kuonekana kama tumekuwa wabinafsi na kwamba hatutaki ndugu. Nina uhakika nyakati ukikua kwenye familia yako wako watu walioishi kwenu na kukulia hapo ingali hawakuwa ndugu wa damu. Si kwamba wazazi wako walikuwa wakalimu kuliko wewe hapana, kilichotokea ni kupungukiwa na chakula cha kutosha, hivyo pesa inakuwa na matumizi makubwa mwisho tunashindwa kuishi na ndugu.

Ushauri wangu, moja, bei za pembejeo na mbolea zikishuka, Watanzania wengi watajihusisha na kilimo hata hiki cha msimu. Pili, Wizara ya Viwanda na Biashara ihakikishe masoko ya ndani na nje yanapatika ili wale watakaozalisha na ziada wauze wapate pesa za matumizi. Tatu, maeneo yote ambayo yana mito na maziwa iwekwe miundombinu ya umwagiliaji ili hayo maeneo yaajiri vijana wengi na kutupatia chakula cha kutosha.

Mwisho, maendeleo ni matokeo ya jitihada na maarifa hivyo lazima tufanye kazi sana lakini kwa kutumia maarifa na si mazoea. Nikutakie kazi njema.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Unamkumbuka Wajadi Fundi na wenzake?



Na Adam Fungamwango

**Halafu watu hao walikuwa na tabia ya kusalimiana wenyewe kwa wenyewe. Ni wale ambao huwa wanatuma mara kwa mara. Hii ilisababisha watu hao kusikika karibuni kila kipindi cha salamu. Kama kadi yake haikusomwa basi atasalimiwa. Na kwa sababu hiyo mtu huyo anaweza akasikika kutwa nzima kwenye vipindi vya salamu.**

DUNIA inakwenda kasi sana. Leo hii watu hawasalimiani kwa barua kama ilivyokuwa zamani. Siku hizi mitandao ya kijamii ya aina mbalimbali imechukua mkondo wake. Watu wanachati moja kwa moja, tena si kama wako Tanzania tu hata mmoja akiwa Bongo na mwingine Marekani. Kitakachowatofautisha ni saa tu ya sehemu nasehemu.

Hivi sasa watu wanaweza kujiunga hata kikundi, wakaanza kujadili vitu mbalimbali kama mpira, siasa na muziki sehemu wanayosihi, mikoa walikotoka na hata ya nchi kwa ujumla.

Haikuwa hivyo zamani. Hata kwenye vyombo vya habari, hasa redio watu walikuwa wanasalimiana kupitia kadi za posta, maarufu kama postakadi.

Walikuwa wakizinunua posta na kuandika majina ya watu ambao wanataka kuwasalimia, wanaweka stempu na kuzitumbukiza kwenye kisanduku kabla ya kupelekwa Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD), kusomwa.

Postakadi hizo hizo zilikuwa zikisomwa mara nyingi kwenye kipindi maalum vya salamu kama vile 'Asubuhi Njema', 'Jambo', 'Mchana Mwema', 'Pole kwa Kazi', 'Jioni Njema' na vinginevyo.

Mtu yoyote tu anaweza kuchukua kadi na kuandika, akasalimia yoyote yule, lakini kulikuwa na watu ambao wao walikuwa kama vile ndiyo kazi yao ya kila siku. Kazi yao kubwa ilikuwa kununua postakadi nyingi na kusalimia watu wengi na kuzituma.

Halafu watu hao walikuwa na tabia ya kusalimiana wenyewe kwa wenyewe. Ni wale ambao huwa wanatuma mara kwa mara. Hii ilisababisha watu hao kusikika karibuni kila kipindi cha salamu. Kama kadi yake haikusomwa basi atasalimiwa. Na kwa sababu hiyo mtu huyo anaweza akasikika kutwa nzima kwenye vipindi vya salamu.

Watu hawa wataitwa Mabingwa wa Salamu. Ilikuwa kila ukiamka utawasilia, akisalimia na kusalimiwa. Na ukitaka kusalimua, ni lazima uwasalimia mabingwa hao.

Kwa sababu hiyo watu hao wakawa maarufu sana na kuzeleka hata kwenye midomo na vichwa na wasilizaji wa redio hiyo, wakati huo ikiwa moja tu.

Ikumbukwe kuwa kuna awamu mbili ya mabingwa wa salamu. Kuna ile iliyokuja baada ya ujio wa redio binafsi, ikiwamo Radio One, ambapo, pamoja na kusomwa na postakadi, pia ndipo ilipoanza teknolojia na mtu kupiga simu moja kwa moja na kusalimia laivu.

Awamu ya kwanza ya watuma salamu maarufu ya RTD, inaanza na mtuma salamu maarufu kabisa ambaye sidhani kama kuna mtu anayewafahamu watu hao watataja majina ya watu watatu bila kumtaja yeye. Huyo ni Wajadi Fundi wa Mahuta Shimoni, Newala.

Wengine ambao walikuwa maarufu miaka ya 1980 hadi miaka ya 1990 ni Issa Hasaan Majeshi, Chivalavala M Chivalavala, Limonga Jastin Limonga, Dua Wajadi, Maalim Shaaban Uledi, Mungwangwa wa Mungwangwa, Ngariba Jongo, Kunguru Mwoga, Damas Lusinde Ng'ingo, Nyembo Juma Nyembo, Uwesu Mbuzi, Ubwa Kombo, Nuru Mtoto, Boko Man, Hawa Kilongo na TX Exaud Nnko 'Surambili'.

Wengine ni Samwaja wa Samwaja, Kuwayawaya S Kuwayawaya, Juma Ramadhani Kamage, Ali Mbondei, Zamlata Jongo, Muungwana Zomboko, , Zacharia Ndemfoo, Lukengelo Duma wa Turiani, Mathias Fungaatemu wa RTC Babati, Thomas Mushi Kimboka, Thomas Myani, Kangoma H Kangomba, Dereva Abdallah Mgeni, Abdallah Mpanjinji na Dk. Maulidi Tego.

Hawa si tu kwamba walikuwa wanasalimiana, lakini kua taarifa kuwa walikuwa wanatembeleana na kusaidia. Bingwa wa salamu kutoka Tanga anaweza kwenda Kigoma kumtembelea mwenzake huko na kukaa huko hata wiki mbili kwa gharama na mwenyeji wake.

Baada ya enzi wa postakadi, ikaja sasa mwishoni mwa miaka ya 1990 na mwanzoni mwa 2000, mabingwa walikuwa wakipiga simu moja kwa moja na kutuma salamu.

Hapa sasa kikaja kizazi kingine cha mabingwa wa salamu ambao wengi bado watu wana kumbukumbu nao.

Hao ni John Zenze, Ndilana Mwambi, Jangala Kikongosi, Stephen Ishengoma, Bongo Experience, Juma Msurvivor, Teddy Big Mama, Manka Mushi, Papa Osama, Frank Malecela 'Mubosi', Manase Muhaha, Emma Kulaya, Jumanne Sebarua Tingisha na Chesco Mzee wa Matunda.

Pia wamo Manyota Top Manyota, Lawena Nsonda, Suzi Ngodoki na mtu mmoja mwenye mbwembwe Kung'ombe Chacha Werema Sukari Muhiri Obare. Mtangazaji akimwita Muhiri Obale ataitia hata dakika nzima kwa kuivuta herufi A 'Naaam'.

Hizi ndizo zilikuwa burudani za Mabingwa wa Salaam enzi za postakadi na baadaye simu za moja kwa moja za mezani.

# HADITHI

MILIO mitatu ya risasi ilisikika maeneo ya Keko Bora jijini Dar es Salaam. Sauti hizo za risassi zilifanya watu kutimua mbio na kutafuta chaka la kujificha. Kila mmoja alidhani ni majambazi waliovamia kwa ajili ya kupora pesa dukani au kwenye vibanda vya mawakala wa kampuni za simu. Haikuwa hivyo. Aliyedhaniwa kuwa ni jambazi alichofanya ni kumpora mwanamke mtoto mwenye umri wa mwaka mmoja tu na kuondoka naye akiwa kwenye gari aina ya IST. Huyu jamaa aliyefanya hivyo ni nani? Ni kwa nini aliyemteka mtoto? Mtoto ni wa nani? Mwanamke aliyeporwa mtoto anamfahamu mporaji? Fuatilia kisa hiki kitamu, cha kusisimua na kuhuzunisha.

# Nina Jambo Langu-11

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Enhee, mmefikia wapi?" Aliuliza.

"Jerry, ni kwamba nimeongea na mwanamke mwenzangu. Tumeongea mengi sana. Kusema kweli ni mtu mzuri na mwelewa sana. Amenipa ushirikiano mkubwa na kasema atazidi kunipa ushirikiano huko mbele ya safari." Alisema Ester alionekana mchangamfu zaidi kuliko mwanzo alipokuja.

"Eti Neema ni ya ukweli hayo?"

"Ni kweli, ameniambia mtoto yupo kwao. Tumeongea mengi. Tumeongea kila kitu. Mimi nimeshukuru kwa sababu amenihakikisha kuwa mtoto ni mzima, tena wa afya na alikuwa alimlea kama mama." Neema alijibu.

"Vizuri. Sasa ngoja nikuambie kitu Ester ambacho ulikuwa hujui. Ni kwamba siku mtoto alivyotekwa mikononi mwa mama yake pale kituoni mimi nilishuhudia na nilikodisha bodaboda hadi nyumbani kwenu pale. Kwa hiyo hata siku uliponiita kwenu na kuomba ushauri ambao sikuujua, lakini ulivyonipeleka nilijua ni nyumba ile ile alipoingia Diana. Tayari tulikuwa na mpango wetu na Neema jinsi gani ya kumpata mtoto, lakini Munngu si Athumani limetokea hili."

"Kumbe ndiyo maana hata hukuwa unashangaa wala wasiwasi, na majibu yalikuwa mepesi tu kuwa nitamrudisha mtoto kwao, usiwe na wasiwasi na wala hamtokamatwa, kumbe ulikuwa unajua kila kitu na ulijua utamrudisha kwa nani ambako tutakuwa salama." Ester alionyesha mshangao.

"Ndiyo maana yake." Alijibu kwa Jerry kwa kifupi.

"Jerry na Neema, ninachoomba hapa kwa sasa tuondoke twendeni kwetu Ubungo ili tukamuone mtoto, halafu nimkabidhi mama yake. Ninachotaka pia na yeye akufahamu nyumbani kwa sababu bado kuna jambo letu hatujalimaliza."

Kilichotokea hapo ni kicheko kutoka kwa wote watatu.

"Yaani mmeshaungana na mimi tena mmeniweka pembeni. Haya bwana."

"Tena ukae pembeni kabisa, wewe utakuwa dereva wetu tu, kila kitu sasa tutamaliza wenyewe."




**"Mama Diana, usitake kunifanya mimi mtoto mdogo sana. Nimekuzidi miaka mingi. Mimi nina uchungu na mtoto kuliki hata wewe. Lakini kila mtu anajua kuwa mtoto alitekwa. Na mimi na wewe wote tulikuwepo.**

Neema naye alidakia na vicheko vilizidi kuliko vya mwanzo.

******************************

"Enhee, niambie huyo mtoto umemwokota wapi?" Ni sauti kali ya Benson ikimwuliza mkewe Neema, baada ya kurejea kazini na kumkuta akiwa amembeba mtoto Diana, baada ya kumaliza kumnywesha uji.

"Nimemwokota?" Neema aliuliza kwa mshangao.

"Haya, hujamuokota. Umemtoa wapi wakati alikuwa ametekwa."

"Sasa baba Diana, badala ya kufurahi kwanza mtoto amerudi, tena akiwa hai, wewe unauliza kwa ukali. Kwa hiyo hukutaka arudi?"

"Mama Diana, usitake kunifanya mimi mtoto mdogo sana. Nimekuzidi miaka mingi. Mimi nina uchungu na mtoto kuliki hata wewe. Lakini kila mtu anajua kuwa mtoto alitekwa. Na mimi na wewe wote tulikuwepo. Leo hii eti nikuone tu amerudi kirahisi hivi kweli, bila msaada wa polisi au wasamaria wema kweli. Ina maana walikwita na kukukabidhi au walikuletea mtoto mpaka hapa?" Ben bado alionyesha kutoridhika na jinsi mtoto alivyorudi.

Hakuonekana kuwa na tatizo lolote. Diana alionekana na afya njema. Kakupigia simu na mkewe kuwa mtoto amepatikana au kuna mtu kamwambia ameonekana sehemu fulani.

Ben alichofikiria kuwa mtekaji wa kweli angewapigia simu kutaka pesa. Na angetaka zikawekwe sehemu fulani na mtoto atapatikana sehemu fulani. Na hata kama angetaka kumrudisha bila kutaka pesa, basi angewapigia simu polisi au wazazi na kuwaambia mtoto wao wamemtupa au kumtelekeza sehemu fulani.

Ile shaka aliyokuwa nayo sasa aliyaona yana asilimia kubwa ya ukweli.

Haiwezekani mtoto aliyetekwa na mtu aliyeonekana katili, tena kwa kutumia nguvu kubwa ya risasi, kupatikana kirahisi na mama yake kama vile amekwenda kumchukua nyumba ya jirani alikokwenda kumuweka kwa muda ili aende sokoni.

"Nilishasema wewe mwanamke ni kahaba. Nilishasema kuwa wewe una mwanaume ambaye huenda alikuwa na wasiwasi kuwa mtoto huyu ni wa kwake. Ukamkatalia. Akaamua kumteka na kwenda kumpima DNA. Sasa labda kaona si wake kakupigia simu kukurudishia, au umekwenda kumuomba kwa ajili ya kulinda ndoa." Aliongea Ben kwa sauti kali, macho yakiwa yamemtoka.

"Una uhakika na hicho unachosema baba Diana."

Ben alicheka kicheko ambacho si halisi. Kicheko cha dharau, kilichochanganyikana na hasira.

"Kama si hivyo hebu niambie mtoto umemtoa wapi? Kwa sababu huko ulikomtoa, au hao waliokupa ndiyo waliomteka. Kinachotakiwa ni kwamba hao watu wakamatwe kwa kosa la utekaji. Wewe unawaachaje?"

"Sina haja ya kuwakamata, mimi nimempata mtoto wangu mzima basi, nashukuru Mungu."

"Nani amekupa huyu mtoto na wapi?"

"Baba Diana ungekaa kwanza, ukatulia, mimi ningekueleza kila kitu, sasa wewe umeingia tu naona mwenzangu umekuwa na hasira..."

"Siyo Hasira" Ben alimkatisha mkewe.

"Haiwezekani mtoto katekwa, halafu apatikane kirahisi namna hii kama si wewe na huyo mtekaji hamfahamiani."

Ugomvi huu ulizuka baada ya Neema, Ester na Jerry kwenda Ubungo kumchukua mtoto Diana.

Neema aliwahakikishia usalama kuwa hatakwenda polisi kushtaki na hii ilichagizwa pia na mkasa mzima ulivyokuwa. Ni mkasa ambao hauhitaji kwenda polisi. Waliamua kuumaliza wenyewe Neema na Ester kwa msaada wa Jerry.

"Sasa nasema hivi. Mimi napiga ripoti polisi na kuwaambia kuwa mtoto amepatikana. Lakini sijui amepatikana vipi, yupo mikononi mwa mama yake na hataki kusema ameletwa vipi na ni nani aliyemkabidhi, halafu waje kukuchukua ndiyo utawaambia vizuri."

"Piga. Na mimi ndiyo nawataka hao polisi waje hapa. Na nikiondoka hapa, ndiyo hunioni tena."

"Unafikiri mimi naogopa hilo. Kama hujaniambia nani amekupa huyo mtoto, ina maana hiyo ni tiketi mimi kukuacha." Ben aliongea huku akimsogelea mkewe.

"Ndicho nilichokuwa nataka hicho."

"Nini?"

"Talaka?" Kilichofuatia hakikuwa talaka. Ila ni kibao kikali shavuni kwa Neema kilichomfanya aone nyota nyota.

"Utaniambia na leo utanionyesha huyo hawara yako aliyokupa huyo mtoto." Wakati maneno hayo yanamtoka Ben, alikuwa tayari ameshamchakaza mkewe kwa makofi manne.

Wakati huo Diana alikuwa ameshalazwa kitandani. Amelala usingizi.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# AMBER LULU KAGOMA KUMTAJA ALIYEMPA UJAUZITO

KWA mara ya kwanza, msanii wa BongoFleva, Amber Lulu, amejitokeza hadharani kuonesha ujauzito wake.

Katika sherehe ya 'Baby Shower' yake iliyofanyika maeneo ya Mikocheni ambayo ilihudhuriwa na mastaa mbalimbali wa kike, Amber Lulu amesema anafurahi kuelekea kuwa mama, lakini hamfahamu nani aliyempatia ujauzito huo.

"Nijasikia vizuri kwa sababu naenda kuwa mama mpya mjini na kuna vitu vingi ambavyo vimebadilika na nahitaji kuvifanya, mimi mwenyewe baba wa mtoto simjui ila yupo na sio P Funk Majani, labda msubiri nikijifungua" amesema Amber Lulu.

## Mwana FA aomba radhi 'Dume Suruali'

BAADA ya miaka mitano tangu kutoka wimbo 'Dume Suruali', mwanamuziki na mbunge wa Mwana Fa, ameibuka na kuomba radhi kutokana na kile alichoimba kwenye kibao hicho.

Katika wimbo huo ambao amemshirikisha Vanessa Mdee, ulikuwa na maneno yanayosema "Nihonge nanunua nini, kwanini yani? kuna kipi nisichokijua au ina TV ndani"

Kama kumkumbushia shabiki yake mmoja aliweka maneno hayo katika akaunti ya Twitter, na ndipo Mwana FA, alipojitokeza na kumwambia kipindi hicho alikuwa mdogo na asamehewe.

"Nilikuwa mdogo na mjeuri, mnisamehe" ameandika Mwana FA.



## Vidume mmemsikia Gigy Money?

UMESIKIA haya ya Gigy Money? Basi wewe kama kidume unaweza kujisogeza kwa mrembo huyo, na kama akikuelewa zawadi ya mtoto itakuhusu.

Mwanamuziki huyo ambaye hakosi vituko, amesema kama akimpenda mwanaume, ana uwezo wa kumzalia hata kama akiwa mlemavu na kuhusu kumlea aachiwe yeye jukumu hilo.

"Siwezi kumuacha mwanamume anayenipenda, kunijali na kunipa ninachokitaka japo kuachana kupo pale inapotokea, bado natafuta mapenzi ya kweli kwa sababu mimi nikimpenda sana mwanaume namzalia hapohapo na hata akiwa mlemavu bado nina uwezo wa kumlea kama kawaida" amesema Gigy Money.



HABARI MICHEZO

# Tuchel akumbuka kipigo cha United

**LONDON** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amekubali kwamba kufungwa na Manchester United akiwa na PSG katika hatua ya 16-bora kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya ni kipigo kibaya katika kazi yake.

Machi 2019, United walitoka nyuma kwa mabao 2-0 kutoka mchezo wa kwanza na kupata ushindi katika dakika za mwisho na kufuzu robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika dimba la Parc des Princes.

"Nakiri baada ya kupoteza nilikuwa gizani kwa siku mbili, sikuweza kuzungumza na na mtu yeyote na sikufikiria kitu chochote zaidi ya kipigo kile," alisema Tuchel.

"Inawezekana ikawa ndio kipigo kibaya zaidi kwangu kwa sababu kilikuja bila kutarajia. Katika kipindi kama hicho. Nilikuwa gizani kwa siku mbili ambazo kocha anapaswa kuwa.

"Hakuna njia unaweza kulinganisha mechi hizi mbili. Nimesema jinsi nilivyojisikia baada ya kupoteza Ligi ya Mabingwa Ulaya. Wote tunajua kipigo ni vigumu kukizoea.

"Ningependa kubadili sasa. Tunapenda mashindano na tunapenda kushinda na tunapenda kupigania, nadhani hicho ndicho tutakachokipata Jumapili," aliongeza Tuchel.





# ARTETA: NINA IMANI NA AUBAMEYANG

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amesema anaamini kwamba, mshambuliaji wake Pierre Aubameyang atafunga mabao mengi.

Msimu huu wa 2020/21, Aubameyang amekuwa akiandamwa na ukame wa mabao jambo ambalo lilikuwa linamuweka kwenye wakati mgumu nyota huyo wa kimataifa wa Gabon.

Arteta amesema kuwa anaamini mapito ambayo alikuwa anayapitia nyota huyo yatapita na kurejea kwenye ubora wake.

Aubameyang alifunga mabao mawili kwenye mchezo wa Ligi ya Europa dhidi ya Benfica ya Ureno na kuiwezesha kufuzu hatua ya mtoano wa timu 16.

Alifunga bao la ushindi kwa kichwa zikiwa zimesalia dakika tatu mpira kumalizika na kuifanya Arsenal kusonga mbele kwa uwiano wa mabao 4-3.

"Bado yupo vizuri na anaweza kufanya mambo mengi ndani ya uwanja, hivyo wakati unakuja ambapo ataweza kufunga na kutupa matokeo mazuri," alisema Arteta akinukuliwa na Skky Sport.

"Namuamini kwa kuwa amekuwa akitengeneza nafasi na anatumia nafasi ndani ya uwanja, hivyo naamini ataendelea kufunga zaidi.

Aubameyang sasa amefikisha mabao 13 aliyofunga kwenye mashindano yote msimu huu.

# *Silva kuwakosa Man United*

**LONDON,** England

MLINZI kisiki wa Brazil na Chelsea, Thiago Silva, anatarajiwa kuukosa mchezo wa leo dhidi ya Manchester United utakaopigwa uwanjani Stamford Bridge kwenye Ligi Kuu England.

Kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel amedhibitisha kumkosa mchezaji huyo katika mkutano wake na waandishi wa habari kuelekea mtanange huo unaotegemewa kuwa mgumu kwa pande zote mbili.

"Amefanya mazoezi mwenyewe uwanjani, nadhani ni maendeleo mazuri" alisema Tuchel.

"Ni hatua kubwa kwake (Silva), hivyo nadhani atajiunga na timu wiki ijayo," aliongeza kocha huyo.

Mechi ya mwisho kukutana baina ya timu hizo mbili mchezo ulimalizika kwa sare ya tasa, mchezo huo ulipigwa Uwanja wa Old Trafford.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI AFUNGUA MLANGO WA KUBAKI BARCELONA

### Kwa mujibu wa gazeti la Marca, sasa klabu hiyo inaweza kumpa ofa ya kubaki, lakini...

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi ameripotiwa kufungua mlango wa kubaki Barcelona, lakini miamba hao wa Ligi ya Hispania, La-Liga, wanakazi kubwa ya kufanya.

**Messi mwenye umri wa miaka 33, aliamua kubaki pale Barca baada ya kuomba kuondoka kabla ya kuanza kwa msimu huu na kisha akabadili mawazo.**

Mshindi huyo wa Ballon d'Or mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na majaliwa yake bado hayajajulikana.

Lakini kwa mujibu wa gazeti la Marca, Messi sasa ameamua kufungua mlango wa kubaki Barcelona na hivyo klabu hiyo inaweza kumpa ofa kubwa zaidi licha ya kukabiliwa na mdororo wa kiuchumi kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Ripoti zinasema kwamba, Barca inataka kuimarisha kikosi chake na wanataka kumshawishi Messi kubaki, ambaye anahusishwa na kuwaniwa na Manchester City.

Usajili wa mshambuliaji wa City, Sergio Aguero, nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland, kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante au mkali wa Liverpool, Roberto Firmino unaweza kuisaidia Barca kuimarisha kikosi chake.

Barcelona imekuwa ikipambana kumbakiza Messi klabuni hapo, huku wagombea wa nafasi ya urais unaofanyika Machi mwaka huu wakijigamba kumbakiza nyota huyo wa kimataifa wa Argentina.

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMUWANIA TORRES

MANCHESTER United inaweza kumgeuka mlinzi wa kati wa Villarreal na Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 24, kama mbadala wa beki wa Sevilla, Jules Kounde mwenye miaka 22. ***(Eurosport)***

### BELLERIN KUONDOKA ARSENAL

MLINZI wa Hispania, Hector Bellerin mwenye umri wa miaka 25, anaweza kuondoka Arsenal kipindi cha majira ya joto kinachokuja kama sehemu ya makubaliano na kocha, Mikel Arteta. ***(ESPN)***

### LIVERPOOL YAMTAKA RODRYGO

LIVERPOOL inafuatilia hali ya straika wa Real Madrid na Brazil, Rodrygo mwenye umri wa miaka 20, ambaye anaweza kuondoka kwa miamba hao wa LaLiga kwa pauni milioni 50 kipindi cha majira ya joto. ***(Diario Gol, via Team Talk)***

### TUCHEL KUMSAJILI HAALAND

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amewashiwa taa ya kijani na klabu hiyo katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland kutoka Borussia Dortmund. ***(Bild, via Sun)***

### CALHANOGLU AWINDWA UNITED

MANCHESTER United itatumia mchezo wao wa Ligi ya Europa hatua ya 16 dhidi ya AC Milan kumuangalia kiungo wa Uturuki, Hakan Calhanoglu mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Express)***

### JULIAN KUMRITHI MOURINHO

KOCHA wa RB Leipzig, Julian Nagelsmann, anataka kuhamia Tottenham, ili kuchukua mikoba ya kocha, Jose Mourinho ambaye yupo mbioni kufukuzwa. ***(Bild, via Express)***

### DORTMUND KUACHIA WACHEZAJI

MIAMBA ya Bundesliga, Klabu ya Dortmund inaweza kuwakatia tamaa baadhi ya wachezaji kutokana na kuyumba kwa uchumi uliosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona. ***(Handelsblatt, via Manchester Evening News)***

### LACAZETTE AWANIA MONACO

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Alexandre Lacazette mwenye umri wa miaka 29, anawaniwa na miamba wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1, Monaco. ***(Mirror)***

### KANE AJIPA MWAKA SPURS

MSHAMBULIAJI wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27, anapanga kubaki Tottenham Hotspur angalau kwa mwaka mmoja zaidi. ***(Telegraph)***

### FREIXA KUSAJILI WAWILI

MGOMBEA Urais wa Barcelona, Toni Freixa amedai ana makubaliano ya kuwasajili wachezaji wawili wakubwa ambao wanataka kushinda Ballon d'Or kama akichaguliwa. ***(El Larguero, via Mail)***

HABARI MICHEZO

## Nyoni akana neno kustaafu Taifa Stars

**Na Adam Fungamwango**

BEKI wa Taifa Stars, Erasto Nyoni, amesema hajawahi kutamka popote pale kuwa ana mpango wa kustaafu kuichezea timu hiyo, hivyo amepokea uteuzi huo kwa mara nyingine, akiwa na furaha kubwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Nyoni ambaye anaichezea Simba amesema kumekuwa na dhana yeye ana umri mkubwa na kwamba anatarajia kustaafu kuichezea timu hiyo, huku wengine wakidai alishawahi kutamka neno hilo, lakini ukweli ni kwamba yeye ataendelea kucheza soka kwa muda mrefu.

"Mimi nashukuru kwa kuitwa na kurudi tena kwenye timu ya taifa. Kwa sasa najiandaa kimwili na kiakili kwa ajili ya kutekeleza tena majukumu ya timu ya taifa.

Kingine ni kwamba asilimia kubwa wanaamini kuwa umri wangu ni mkubwa sana. Ingawa siwezi kuwaambia umri wangu, mimi nawaachia wao tu. Nitakachofanya ni kufanya kazi niliyopewa na kocha. Sijawahi kutangaza kuwa nastaafu kucheza soka Taifa Stars kama inayosemwa, hayo yote nawaachia mashabiki, mimi kazi yangu ni kucheza mpira," alisema Nyoni ambaye anacheza namba zote za nyuma, kasoro kipa, huku pia akiwa na uwezo wa kucheza kama kiungo mkabaji.

## Zimamoto yapania kuzinduka Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA wa timu ya Zimamoto, Juma Abdulrahman, amesema anaimani timu yake itafanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu Zanzibar licha ya kushindwa kufanya hivyo kwa sasa.

Zimamoto ambayo kwa sasa ipo nafasi ya nane ikiwa na alama 14 katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar yenye timu 12, imepoteza michezo minne, sare tano na kushinda michezo mitatu pekee ikiwa ni baada ya juzi kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya vinara wa ligi hiyo, KMKM.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, kocha huyo alisema timu kupata mfululizo wa matokeo mabaya ni jambo la kawaida katika soka na kipindi hicho huitwa cha mpito.

Alisema ni muhimu kwa wachezaji na benchi la ufundi kwa ujumla kushirikiana hususan kwa sehemu zenye upungufu ili kuhakikisha katika michezo inayofuata wanapata ushindi.

"Hatupati matokeo mazuri, tuseme tangu msimu huu uanze, lakini haimaanishi kama tunakata tamaa, hapana kikubwa ni kuendelea kujituma ili kuwatia moyo wachezaji na mashabiki wetu kwa ujumla," alisema.

# MOROCCO AACHIWA UAMUZI WA KUSAJILI NAMUNGO CAF

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, uongozi wa Klabu ya Namungo, umesema suala la usajili wa nyota 10 liko mikononi mwa Kocha Mkuu, Hemed Morocco.

Akizungumza na gazeti hili jijini juzi, Mwenyekiti wa Namungo FC, Hassan Zidadu, alisema wanafurahi kuona timu yao imefanikiwa kuingia hatua ya makundi, hivyo watatumia vizuri nafasi iliyotolewa na Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF) ya kusajili nyota 10 zaidi, lakini hilo wanaliacha chini ya kocha Morocco.

Alisema ni lazima waongeze nguvu kwa kusajili wachezaji ambao watasaidia timu kujiimarisha kuelekea hatua ya makundi.

**Alisema watakapopokea mapendekezo kutoka benchi la ufundi watahakikisha wanayatekeleza kwa kusajili wachezaji ambao anawahitaji katika hatua hii ya makundi.**

Nipashe lilipomuuliza Morocco, alisema anafurahi na kuwapongeza wachezaji wake kwa kupambana kwa kufanikiwa kutinga hatua ya makundi kutokana na ukweli kwamba wao bado ni timu changa katika Ligi Kuu Bara na kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Alisema wamemaliza mechi nne ambazo zimewapa uzoefu na sasa wanaenda kujipanga kwa ajili ya michezo yao ya hatua ya makundi.

"Nimeona timu ambazo tumepangwa nazo katika kundi letu, si rahisi kwa sababu wapinzani wetu ambao tuko nao ni wazoefu, ila tunaenda kufanyia kazi upungufu wetu," alisema Morocco.

Kuhusu usajili, Morocco alisema: "Tutaongeza wachezaji ambao watasaidia timu yetu kufanya vizuri na kufikia malengo yetu ambayo tumeyaweka katika michuano hii."

Namungo ambayo ipo Kundi D pamoja na Pyramids ya Misri, Nkana FC (Zambia) na Raja Casablanca ya Morocco, Machi 10, mwaka huu itaanzia ugenini dhidi ya Wamorocco hao.




Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere (Kushoto), akijaribu kuachia shuti langoni mwa African Lyon FC huku akipata upinzani kutoka kwa beki wa timu hiyo, kwenye mechi ya Kombe la FA hatua ya 32, iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na Wekundu wa Msimbazi hao kushinda 3-0. **MPIGAPICHA WETU**

# *Mwameja amvulia kofia Manula*

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa zamani wa klabu za Coastal Union, Simba na timu ya Taifa, Taifa Stars, Mohamed Mwameja, amemwagia sifa kipa wa sasa wa timu hiyo, Aishi Manula, akidai kuwa ameongezeka uwezo, baada ya kuongezewa vitu fulani.

Mwameja amesema licha ya kwamba Manula anaonekana kuondoa michomo ya hatari langoni mwake, lakini ameisaidia Simba kupata pointi kadhaa kwenye mechi mbalimbali ambazo imecheza na kama si uhodari wake, basi ingezikosa.

"Ameimarika kwenye mechi hizi tatu nilizoangalia, hajaruhusu goli. Na nikiangalia sana pia hata mabeki wa Simba nao wamemsaidia kufanya vizuri, na yeye pia ameisaidia timu kupata pointi tatu," alisema Mwameja ambaye alisifika enzi zake kwa uwezo wake mkubwa wa kudaka na kuokoa penalti.

Mwameja alisema inawezekana ujio wa kocha mpya wa makipa, Mbarzil Milton Nienov, umemuongezea vitu vya ziada ambavyo hakuwa navyo kabla.

"Inawezekana ujio wa kocha mpya wa makipa nao umemsaidia. Si tu kama waliopo siyo wazuri, ila wakati mwingine unapofanya kazi na mtu uliyemzoea kunakuwa na changamoto ya kile unachoelekezwa kutokifanya kwa usahihi," alisema.

Alisema amemuona Manula, tangu kuanza kwa Fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), na kwamba amekuwa kwenye kiwango cha juu, na si yule wa miaka mitatu nyuma.

"Siku zote matokeo ya mechi yanaamuliwa na mabeki na kipa. Beki na kipa wakiwa vizuri kuna asilimia kubwa kutoka na ushindi. Kipa anatakiwa kulinda goli lake mpira usiingie na kuongea na mabeki wake, nampongeza kwa hilo naona yuko kwenye nafasi nzuri ya kuwa mmoja wa makipa bora Afrika na hata kuchukuliwa na timu za nje ya nchi. Na itakuwa vizuri kwa manufaa ya taifa," alisema Mwameja.

Manula hajaruhusu bao kwenye mechi tatu mfululizo za Ligi ya Mabingwa Afrika, dhidi ya FC Platinum ya Zimbabwe, Simba ikishinda mabao 4-0, As Vita ya Congo DR, ikishinda 1-0 na Ahly ya Misri, pia ikishinda 1-0.

Moja ya mchomo mkali aliookoa ambao ulimpa sifa sana ni ule wa dakika za mwisho kwenye mechi dhidi ya Al Ahly, Jumanne iliyopita.

# Michezo




Jumapili Februari 28, 2021
Nipashe

Messi afungua mlango kubaki Barca UKURASA 22

**KITU HICHO...**



Beki wa Kati wa Manchester City, Ruben Dias, akiifungia timu yake bao la kwanza kwa kichwa, akiitendea haki krosi ya Kevin de Bruyne wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya West Ham United, kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Etihad jana. Bao la pili lilifungwa na beki John Stones huku lile la wapinzani likifungwa na Michail Antonio. **PICHA: MTANDAO**

## Simba yageukia 3 za JKT Tanzania

**Na Saada Akida**

BAADA ya kutinga hatua ya 16-bora ya Kombe la Azam Federation (FA Cup), Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, pamoja na kuwapongeza wachezaji wake kwa kujituma na kuibuka na ushindi dhidi ya African Lyon, amesema hesabu zake sasa anazigeuzia katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya JKT Tanzania itakayopigwa kesho, Jumatatu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Temeke mkoani Dar es Salaam.

Simba ambao ni mabingwa watetezi wa Kombe la FA, juzi waliendeleza kasi yao ya kutetea taji hilo kwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya African Lyon katika Uwanja wa Benjamin Mkapa shukrani kwa Ibrahim Ajibu ayecheka na nyavu mara mbili dakika ya tisa na 43 huku Perfect Chikwende akitupia la tatu dakika ya 63.

Kwa ushindi huo Simba sasa itakutana na Kagera Sugar kuwania kutinga robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Gomes alisema licha ya kufanya mabadiliko ya kikosi chake, wachezaji wake walipambana na kupata ushindi na kusonga mbele kucheza hatua ya 16-bora, hivyo sasa akili yake anaielekeza dhidi ya JKT Tanzania kesho.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa, hivyo kila mechi tunahitaji kupata matokeo chanya, tunasahau matokeo ya mechi hii na kujiandaa kwa mchezo dhidi JKT Tanzania, ni mechi ngumu kwa kuwa tunahitaji kupata pointi muhimu ili kujiweka katika mazingira mazuri kwenye mbio za ubingwa," alisema Gomes.

Alisema kuelekea mchezo huo pia atafanya mabadiliko ya wachezaji kwa kuwapa nafasi ya kupumzika nyota wake ambao wametumika kwa muda mrefu.

# FISTON AFUNGUA AKAUNTI YANGA IKIIFUATA KMC FA

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Carlinhos yeye ageuka bondia alimwa nyekundu, sasa kukosa mechi tatu akianza na dhidi ya Coastal...

STRAIKA mpya wa Yanga, Fiston Abdulrazack, amefunga bao lake la kwanza kwa timu hiyo tangu ajiunge nayo kwenye dirisha dogo la usajili Januari mwaka huu, na kuifanya timu yake kushinda 1-0 dhidi ya Ken Gold ya Chunya, Mbeya kwenye mechi ya raundi ya nne ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jana.

**Fiston, raia wa Burundi alifunga bao hilo kwa mkwaju wa penalti dakika tatu kabla ya mapumziko baada ya beki Boniface Mwanjombe kuunawa mpira ndani ya eneo la hatari, akiipeleka timu yake hatua ya 16-bora ya michuano hiyo.**

Kwa matokeo hayo, Yanga sasa itakutana uso kwa uso na KMC ambayo juzi ilitinga hatua hiyo kwenye uwanja huo huo kwa kuichapa Kurugenzi kwa mabao 5-2.

Yanga ilifanya mashambulizi mengi kipindi cha kwanza, huku Ken Gold ikionekana kujilinda zaidi huku ikifanya shambulizi moja tu kipindi hicho katika dakika ya 13 baada Raymond Mwasota kushindwa kuunganisha vizuri mpira uliotemwa na kipa Farouk Shikalo, akapiga juu ya lango wakati likiwa tupu.

Kabla ya hapo, dakika ya 11, Ditram Nchimbi alikuwa ametoka kukosa bao la wazi kwa kupiga shuti nje, baada ya kumegewa pande safi kutoka kwa Fiston.

Fiston pia alikosa bao dakika ya 23, alipounganisha mpira wa faulo, lakini kipa Adam Juma aliupangua na kuwa kona ambayo haijazaa matunda. Kipindi cha pili Yanga iliwatoa Deus Kaseke, Nchimbi na Fiston na nafasi zao kuchukuliwa na Carlos Carlinhos, Haruna Niyonzima na Michael Sarpong.

Ni kipindi ambacho Ken Gold walionekana kuchoka, wakiwaacha Yanga wakicheza soka wanavyotaka, lakini tatizo lao kubwa lilikuwa ni kuukwamisha mpira ndani ya wavu.

Carlinhos alizawadiwa kadi nyekundu ya moja kwa moja dakika ya 80, baada ya kumpiga ngumi Mwanjombe akiwa hana mpira. Kadi hiyo inamfanya kukosa mechi tatu na kanuni zinasema kuwa kadi ya Kombe la FA, inatumika pia kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, hivyo ataanza kuukosa mchezo kati ya timu yake na Coastal Union.

Kabla ya hapo, alikosa bao la wazi dakika ya 67, akiunganisha mpira wa kichwa kutoka kwa Yassin Mustapha, lakini kipa Adam aliudaka kwa ustadi. Dakika ya 90, timu zote mbili zilikosa mabao ya wazi, Zawadi Mauya akijichanganya mwenyewe na kusababisha hatari ambayo wachezaji wa Ken Gold hawakuweza kuwa makini, sekunde chache baadaye, Haruna Niyonzima akakosa bao yeye na kipa.

Ken Gold inayofundishwa na kiungo wa zamani wa Yanga, Salvatory Edrward, ipo Daraja la Kwanza Tanzania Bara, Kundi A, ikipigana kucheza Ligi Kuu msimu ujao, ikiwa inashika nafasi ya tatu kwa pointi 16, ikicheza michezo 10 mpaka sasa.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >